# 'MIKAKATI YA UPOLE YA LUGHA KATIKA MATUMIZI YA LUGHA YA VIJANA'

NA

*Kariithi Francis M*

C50/71973/2008

Kazi hii imewasilishwa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili

( M.A) Kiswahili katika chuo kikuu cha Nairobi

University of NAIROBI Library

0404838 5

JUNI 2010

## UNGAMO

**Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu chochote kile.**

28/10/2010 ..................................

**Tarehe**

.................................. **Francis Kariithi M.**

**Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu.**

28-10-2010 ..................................

**Tarehe**

.................................. **Dkt. K. W Wamitila**

28/10/2010 ..................................

**Tarehe**

.................................. **Dkt. J. Mweri**

*IKISIRI*

Utafiti huu ulilenga kutambulisha mikakati ya upole ya lugha inayotumiwa na vijana katika matumizi yao ya lugha. Vijana wamechukuliwa kama kundi lisilokuwa na hadhari pale linapoitumia lugha katika mazungumzo yanayozungukia miktadha mbalimbali kama vile ya kifo, magonjwa, kazi mbalimbali za sehemu za mwili, maswala ya kujamiiana na kadhalika.

Japo kumekuwa na manung'uniko kuhusiana na matumizi ya lugha ya vijana yasiyokuwa na upole, utafiti wetu ulitarajia kuchanganua matumizi safidi ya lugha katika lugha ya mazungumzo ya vijana na kuthibitisha kuwa kuna upole unaoendana na matumizi ya lugha kwa vijana kwani wanapoitumia mikakati fulanifulani ili kuzuia kumkirihi mtu katika matumizi yao ya lugha, bila shaka huku ni kudhihirisha kuwepo kwa upole.

Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa njia ya matumizi ya hojaji ambayo iliyafumbata maswala ambayo kwa kawaida hupelekea mtumiaji wa lugha kuonekana kana kwamba ni mtu aliyepujukwa na maadili ikiwa ataitumia lugha yake kinyume na matarajio ya jamii.
Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Ili kuthibitisha kuwepo kwa mikakati ya upole ya matumizi ya lugha ya vijana, tuliongozwa na matokeo ya namna watafitiwa walivyokuwa wakiangazia maswala tofauti tofauti kwenye hojaji.

Tuliwateua vjana 30 kutoka kwa shule tatu za manispaa ya mji wa Nakuru ambapo wavulana walikuwa 15 nao wasichana idadi kama hiyo. Matokeo ya uchanganuzi,

yalibainisha bayana kuwa vijana hutumia mseto wa mikakati ya upole katika matumizi yao ya lugha. Ushahidi ulio na mashiko ni kuwa mikakati hutegemea vijana wanawasiliana na nani, mada ni gani na sababu za kuwasiliana ni gani.

SHUKRANI

Ukamilifu wa kazi hii haungewezekana pasipo na mchango wa watu mbalimbali. Kwanza kabisa, nampa mkono wa tahania Mwenyezi Mungu kwa kuniongoza kupitia Roho Wake na kuifanya ndoto hii kutimilika.

Shukrani jazila ziiendee Tume Ya Uajiri wa Walimu kwa kunipa likizo kwenda kusoma huku nikiendelea kupokea mshahara wangu ili kuweza kugharamia masomo haya.
Sijui niseme nini, kama si wewe mke wangu Irene, mambo yangeniendea segemnege. Ulinihimiza, ukanivumilia kwa kero za kukoseshwa usingizi, umekuwa '**kito**' katika maisha yangu. Watoto wangu Rick, Isaac na Charles mlivumilia kwa kutokuwa nami wakati mlinihitaji zaidi.

Dkt. Wamitila na Dkt. Mweri wamekuwa wasimamizi wa kupigiwa mfano, ushauri wao umeufanikisha utafiti huu. Mwenyezi Mungu awe nanyi siku zote za maisha yenu kwani mmekuwa manahodha wema.

Shukrani zingine ziwaendee wahadhiri katika Idara ya Isimu Na Lugha, mioyo yenu safi iliniwezesha kuhusianana nanyi pasipo na pingamizi. Fauka ya hayo, natoa pongezi kwa wahadhiri hawa kwa mchango wao, Dkt Habwe (ulinifaa sana), Dkt Zaja, Dkt Iribe, Dkt Kineene, Dkt Buregeya, Dkt Mbatiah, Dkt Olali, Prof. Abdulaziz, Prof. Mberia, Dkt Schroeder, Bw Mungania na Bi Jerono. Prof. Buliba wa Egerton nasema ahsante kwa ushauri wako, ulinifaa pakubwa.

Wanafunzi wezangu pia sitawasahau, hawa ni Walubengo, Makhoha, Kapufi, Njue, Nasimiyu na Wanjugu. 'Malitotos' wanafunzi wa kiingereza nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu, Mungu awajalie neema yake mpandapo ngazi hii ya masomo.

Mwisho nawashukuru wote waliohusika kwa hali yoyote ile, mlikuwa msaada kwangu wakati wote huo. Ijapokuwa sikuwataja kwa majina, nasema Ahsanteni sana na Mungu awabariki.

# KUTABARUKU

Kwa mamangu mzazi Jane Wanjiru

Marehemu babangu Kariithi Gichuhi.

Malezi yenu na nidhamu mliyodhamini imekuwa dira yangu muda huu wote.

Bishop Marita Charles

Mahubiri yako yalikuwa mbegu iliyoota na kumea ndani yangu. Mungu akuzidishie neema zake pamoja na aila yako.

Familia ya Wan'gan'ga

Mmekuwa chemchemi yangu.

## *YALIYOMO*

*UNGAMO* ........ *i*

*IKISIRI* ........ *ii - iii*

*SHUKRANI* ........ *iv*

*TABARUKU* ........ *v*

*YALIYOMO* ........ *vi – x*

*UFUPISHO wa MANENO* ........ *xi*

SURA YA KWANZA ........ 1

UJENZI WA UTAFITI ........ 1

1.0 UTANGULIZI ........ 1

1.1 Usuli Wa Mada ........ 1 - 3

1.2 Swala La Utafiti ........ 3

1.3 Malengo Ya Utafiti ........ 3 - 4

1.4 Nadharia Tete Za Utafiti ........ 4

1.5 Umuhimu Wa Utafiti ........ 4 - 5

1.6 Upeo Na Mipaka Ya Utafiti ........ 6

1.7 Maelezo Ya Istilahi ........ 7

1.8 Msingi Wa Nadharia ........ 8

1.8.1 Nadharia ya Upole ........ 8 - 17

1.8.2 Mahitaji ya uso ........ 17

1.9.0 Mapitio Ya Maandiko ........ 18

1.9.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 18 - 22

1.10 Mbinu Za Utafiti ........ 23

1.10.1 Uteuzi wa watafitiwa ........ 23

1.10.2 Ukusanyaji wa data ........ 23

1.10. 3 Vifaa vya ukusanyaji wa data ........ 23 - 24

1.10.4 Uchanganuzi wa data ........ 24

1.11 Hitimisho ........ 24

## SURA YA PILI

### MAELEZO YA LUGHA KUHUSIANA NA MIKAKATI YA UPOLE KATIKA MATUMIZI YA LUGHA

2.1 UTANGULIZI ........ 25

2.2 Lugha Ya Kitamathali ........ 25 - 27

2.3.1 Mtazamo Wa Grice Wa Uhusishaji ........ 27 - 29

2.3.2 Uhusishaji ........ 29 - 31

2.4. Kuchanganya Na Kuhamisha Ndimi ........ 31

2.4.1 Kuchanganya ndimi au msimbo ........ 31

2.4.2 Kuhamisha ndimi au msimbo ........ 32

2.4.3 Tasifida kama msimbo ........ 32 - 33

2.5 Uchaguzi Wa Kileksika kama mkakati ........ 34

2.5.1Utaratibu wa uchaguzi wa neno ........ 35

2.6 Mazungumzo Ya Mzunguko ....................................................35 - 36

2.6.1Nadharia ya Uso ....................................................................... 36

2.6.1 Ujumbe unaowasilishwa ................................................. 36 – 39

2.6.3Majukumu ya mazungumzo ya mzunguko katika

Mawasiliano ................................................................. 39

2.6.4 Kukiukwa kwa kanuni za Grice za kushirikiana .......................... 39

2.6.5 Ubabe na umoja ........................................................................ 40

2.6.6 Mzaha kama maelezo ya mzunguko ............................................ 40

2.7 Lugha Na Utamaduni kama dira ....................................................40 - 42

2.8 Vichocheo vya uchaguzi Wa Mkakati ...............................................42 - 43

2.9 Hitimisho.......................................................................................44 - 45

SURA YA TATU

MIKAKATI YA UPOLE KATIKA MATUMIZI YA LUGHA YA VIJANA.

3.1 Utangulizi.................................................................................... 46

3.2. Mielekeo ya vijana kuzihusu methali ............................................... 47

3.3 Mikakati ya lugha kati ya vijana na wazazi wao .............................48 - 50

3. 4 Mikakati ya lugha kati ya vijana na walimu.............................. 50 – 52

3.5 Mikakati ya lugha kati ya vijana na marafiki zao ......................... 52 – 54

3.6 Mikakati ya lugha kati ya vijana na

watu wasiowajua ........................................................................54 - 55

3.7 Mikakati ya lugha kati ya vijana na watoto, daktari

na mgonjwa wa Ukimwi.............................................................55 - 56

3.8 Mikakati ibuka katika matumizi ya lugha ya

Vijana katika utafiti .................................................................56 -57

3.8.1 kuchanganya / Kuhamisha ndimi ............................................57

3.8.2 Vijana na ubadilishaji / uchanganyaji

wa ndimi..........................................................................57 - 59

3.8.3 Vijana na matumizi ya misimbo.............................................59 - 60

3.8.4 Tasfida kama mkakati wa upole.............................................60 - 61

3.8.5 Lugha Ya Mzunguko ...........................................................61 - 64

3.8.6 Maongezi na uhusishaji.......................................................64 - 66

3.8.7 Lugha ya kitamathali kama tasifida katika

matumizi ya lugha ya vijana ..............................................67 - 68

3.8.8 Utafutaji wa fadhila............................................................68 - 69

3.9 Hitimisho.................................................................................... 69

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA MATOKEO YA TOFAUTI YA MATUMIZI YA MIKAKATI YA UPOLE KWA VIJANA

4.1 Utangulizi ........................................ 70

4.2 Uwepo wa Uso katika ujana ........................................ 70 - 72

4.3 Vijana na wazazi wao ........................................ 72 - 77

4.4 Vijana na walimu wao ........................................ 77 - 80

4.5 Vijana na marafiki zao ........................................ 80 - 85

4.6 Vijana na watu wasiowajua ........................................ 85 - 88

4.7 Vijana na watoto wadogo mgonjwa na daktari ........................................ 89 - 93

4.8 Hitimisho ........................................ 93

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO ........................................ 94

5.1 Utangulizi ........................................ 94

5.2 Muhtasari Wa Matokeo ........................................ 94 - 96

5.3 Mipaka Ya Utafiti ........................................ 96

5.4 Rai Kwa Utafiti Zaidi ........................................ 97

MAREJELEO ........................................ 98 – 102

KIAMBATISHO ........................................ 103 - 107

5.1 Utangulizi ........................................................................................94

5.2 Muhtasari Wa Matokeo................................................................94 - 96

5.3 Mipaka Ya Utafiti ........................................................................................96

5.4 Rai Kwa Utafiti Zaidi ........................................................................................97

MAREJELEO ........................................................................................98 – 102

KIAMBATISHO ........................................................................................103 - 107

## Ufupisho wa maneno

| | |
|---|---|
| Wtf | Watafitiwa |
| Jml | jumla |
| K.h.j | kama hapo juu |
| N. k | na kadhalika |

# SURA YA KWANZA

# UJENZI WA UTAFITI

## 1.0 UTANGULIZI

Kazi hii imegawika katika sura tano: sura ya kwanza imeshughulikia ujenzi wa somo la utafiti. Hapa pia mtafiti ananuia kuelezea azma yake kuu au kichocheo na msukumo uliompa ilhamu kiasi cha kutaka kufanya utafiti kuhusiana na mada hii, vilevile katika sura hii tumehakiki kazi mbalimbali zenye uhusiano na utafiti wetu na nadharia iliyotumika katika utafiti huu. Katika sura ya pili, tumeangazia mambo ya kimsingi kuhusiana na matumizi ya lugha katika mawasiliano yanayoendana na mikakati ya upole katika lugha. Sura ya tatu tumetambulisha mikakati iliyoibuka katika utafiti pamwe na vile watafitiwa walizijaliza hojaji. Sura ya nne imeweza kubainisha tofauti iliyopo kati ya mikakati husika kwa kudhihirisha viwango kuhusiana na kila swala. Mwisho tumetamatisha na kutoa mapendekezo yetu katika sura ya tano.

## 1.1 USULI WA MADA

Vijana ni sehemu moja muhimu katika jamii kwani ndio ambao wanaunganisha kizazi cha chini na kile cha juu hivyo basi kutolishughulikia kundi hili ni sawa na kutoijali kesho ya watoto wetu. Kutokana na mtagusano uliopo baina ya vijana katika shughuli zao za kila siku, na jamii nzima kwa jumla, welewa wa mikakati ya upole inayotumiwa na vijana katika matumizi ya lugha wanapokumbana na maswala yanayokirihi ni muhimu mno. Maswala yenye kuzua kero katika matumizi ya lugha ni mambo ambayo hayawezi yakatengwa na jamii hivyo basi uchanganuzi wa mikakati ya upole wanayotumia kuisafidi lugha itaisadia

jamii kuelewa vijana wake na hivyo basi kurahisisha upashanaji wa habari. Kuielewa mikakati hii ya upole ya matumizi ya lugha ya vijana kutapelekea kurahisisha mawasiliano katika jamii na kulielewa kundi hili; hatimaye kuafikia mwafaka katika mambo fulani, ikumbukwe kuwa kulingana na *Youth Challenge International (2009)* asilimia sitini ya idadi ya watu nchini Kenya ni ya vijana kati ya miaka 15 na 35, na asilimia sitini na moja ya vijana nchini Kenya haijaajiriwa; huku ni kumaanisha kuwa idadi kubwa ya watu ni ya vijana. King'ei na Kobia (2007:325) katika jarida la *Nordic Journal of African Studies* wameshikilia msimamo huo huo kuwa zaidi ya asilimia 60% ya idadi ya watu nchini Kenya ni vijana; hivyo basi kuwaelewa kutamaanisha kuyaafikia maazimio mengi ya jamii na utangamano katika maswala mengi yanayoihusu jamii.

Msukumo ambao umenipelekea kutaka kuitafiti mikakati ya upole ya vijana ya matumizi ya lugha ni kutokana na ukweli kuwa vijana wametokea kupuuzwa na viongozi na jamii nzima kwa jumla, ili kuwaelewa vizuri kuna haja ya kuichanganua mikakati ya upole wanayoitumia katika lugha yao. Wardhaugh (1986:237) anasema huenda lugha ikasafidiwa kwa kuyaepuka maneno yenye makali, kutokea na msimbo wao wenyewe, kutumia lugha nyingine isiyoonyesha makali au hata kuzungukia mbali kuelezea dhana iliyoko karibu.

Fromkin na wenzake (2003:487) wanasema kuwa, 'duniani kote na katika historia watu wamebuni lugha ya siri na michezo ya lugha. Wametokea kuitumia lugha hii aidha kama kitambulisho mahususi cha kikundi fulani... ama kama njia ya kuwafanya wengine wasipate kuelewa kile kinachosemwa.' Vijana katika jamii yetu huenda wakawa na mikakati ya aina

hii, welewa wake utakuwa dawa mjarabu katika kulielewa kundi hili kwa ukamilifu wake. Welewa wa mikakati ya upole wanayotumia katika lugha kutapelekea wazazi na washauri wengine kupata nafasi murua ya kurahisisha mawasiliano kati ya vijana na makundi mengine ya jamii na kuafikia mwafaka fulani kwa ukamilifu. Maswala nyeti katika jamii ni kama vile kazi za sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu, shughuli za kujamiiana, maswala ya kifo, magonjwa, umasikini, maswala ya fedha n. k.

## 1.2 SWALA LA UTAFITI

Kumekuwa na manung'uniko juu ya namna vijana wanavyotumia lugha katika kuwasilisha ujumbe, hususan juu ya mada ambazo zinafikiriwa na jamii kuwa nyeti. UNESCO (2004) waliangazia maswala kadha kuhusiana na lugha ambapo:

- *Wanaiona lugha kama tukio badalia la vurugu katika mawasiliano, na*
- *Vurugu kama tukio la kila siku katika matumizi ya lugha (TY).*

Imedaiwa kwamba katika mkabala huu lugha ya vijana huwa haina upole na hudhihirisha upungufu wa nidhamu wanapowasiliana na makundi tofauti tofauti katika jamii; ni katika misingi hii ndipo utafiti huu unanuia kuchunguza mikakati ya upole ya lugha katika matumizi ya lugha ya vijana.

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI

- Kutambulisha matumizi ya mikakati ya upole ya lugha inayotumiwa na vijana kuzungumzia maswala yanayokirihi.

- Kuchanganua matumizi ya mikakati ya upole ya lugha katika mazungumzo ya vijana.
- Kuchanganua tofauti ya matumizi ya mikakati ya upole ya lugha katika mazungumzo ya wavulana na wasichana.

## 1.4 NADHARIA TETE ZA UTAFITI

- Vijana hutumia mikakati ya upole ya lugha kuangazia maswala nyeti katika matumizi yao ya lugha wanapowasiliana.
- Kuna matumizi ya mikakati ya upole ya lugha katika mazungumzo ya vijana.
- Kuna tofauti katika matumizi ya mikakati ya upole ya lugha katika mazungumzo ya wavulana na wasichana.

## 1.5 UMUHIMU WA UTAFITI

Lugha hufumbata maswala yote ya jamii, hivyo basi ni kupitia matumizi ya lugha ambapo tunajifunza tamaduni za jamii zetu. Ni kupitia lugha ambapo imani na mawazo ya jamii hurithishwa kizazi kingine. Kuwepo na mikakati ya matumizi ya lugha katika jamii ni jambo moja ambalo hujitokeza katika jamii. Trudgill (2002) anasema kuwa, 'thamani ya jamii huenda ikawa na athari kwa lugha yake.... '

Kutokana na maelezo haya utafiti wetu unapata msukumo kwani vijana huchukua nafasi muhimu katika jamii na tukio la kutoangazia mikakati ya upole ya lugha ambayo wao hutumia katika lugha kutaashiria jamii isiyo na nafasi kwa vijana wake.

Wachiuri (2005) ametaja kuwa warsha iliyokuwa inatarajiwa kutoa mwangaza juu ya mahusiano ya lugha na kusambaa kwa ugonjwa wa UKIMWI ilitokea kutoafikia malengo yake kwani waliohudhuria warsha hiyo walidai kuwa msamiati ulikuwa unazua utata na ulileta wingu la giza. Wachiuri (k.h.j) alitokea na mapendekezo kuwa mikakati ya kuwasiliana na vijana ibadilishwe. Tafiti nyingi ambazo zimefanywa hapa zimetokea kutoliangazia swala la matumizi ya lugha kwa vijana hivyo basi kuashiria kuwepo na pengo kubwa ambalo tunadhamiria kulijaza.

Kutokana na swala la matumizi ya lugha miongoni mwa vijana kutopewa uzito wa kutosha, kwanza kuna umuhimu wa kuielewa mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana na pili kubainisha kuwa vijana wana njia mbalimbali za kudhihirisha matumizi ya upole katika lugha yao.

Huenda welewa wa mikakati ya upole ya matumizi ya lugha ya vijana katika jamii yao kutachangia katika kuwahamasisha juu ya maswala yanayokirihisha. Isitoshe, ikiwa mikakati ya kusafidi lugha katika matumizi ya lugha ya vijana ipo, washauri wa vijana watakuwa na wakati mwanana wa kuwasiliana na vijana kwani hii itakuwa hatua moja muhimu ya kuyaafikia malengo kwa yeyote mwenye nia njema kwa vijana wetu.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu uliazimia kuchunguza namna vijana hutumia mikakati ya upole katika matumizi ya lugha katika mawasiliano yao. Vijana tuliotarajia kutumia ni wale wa shule za sekondari katika Manispaa ya Nakuru ambapo vijana wa jinsia zote waliteuliwa. Manispaa ya mji wa Nakuru ilichaguliwa kwa sababu shule za sekondari haziko mbalimbali na hivyo basi kuurahisisha ukusanyaji wa data vilevile kutokana na makabila tofauti kupatikana katika eneo hili, data yetu itatoa mchango kwa utafiti mwingine kwani vijana walikuwa ni mseto wa watafitiwa tofauti. Tulitumia wanafunzi wa kidato cha nne ambapo uteuzi ulikuwa wa kimakusudi na si kwamba kulikuwa na jambo ambalo lilikuwa limechochea uamuzi huu.

Shule ambazo tuliziteua vilevile ziliteuliwa kimakusudi ambazo ni Lake Lawrezzo, Menengai High na Afraha Secondary. Shule hizi haziko mbalimbali na hivyo basi ziliurahisisha ukusanyaji wetu wa data. Wanafunzi 10 kutoka kwa kila shule walihusishwa. Utafiti wetu ulitekelezwa kwa kutumia hojaji. Tulichanganua matokeo ya vile watafitiwa walikuwa wametumia mikakati ya upole katika lugha yao. Tofauti baina ya wavulana na wasichana ilitathminiwa ili kubainisha kama upole katika matumizi ya lugha baina ya makundi haya mawili yanatofautiana.

## 1.7 MAELEZO YA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Lugha miiko | TUKI (1990:38) kaida za kuepuka matumizi ya maneno yenye hisia mbaya au kali kwa kutumia tasifida mbalimbali. |
| Mkakati wa upole | Utaratibu unaotumiwa ili kuafikia malego fulani na mtu. |
| Uso chanya | Mkakati unaojaribu kupunguza tishio la kuudhuru uso wa anayekusikiza. |
| Uso hasi | Mkakati ambao unadhamiria kuutishia au kutoutishia uhuru wa msikilizaji |
| Kuwa kwenye ya rekodi | Mkakati ambao haujishughulishi kupunguza tendo la kuutishia uso wa msikilizaji japo kunazo njia za kudhihirisha upole zinazoendana na hali hii. |
| Kuwa nje ya rekodi | Mkakati unaotumia lugha ya mzunguko ambao humwondolea mzungumzaji uwezekano wa kumlazimishia msikilizaji jambo. |
| Mahitaji ya uso | Matarajio kuwa mitazamo ya umma kuuhusu uso wa mtu itaheshimiwa. |
| Tendo la kutishia uso | Jambo lolote lisemwalo na ambalo linadhuru mtu au kumkirihisha na kuupuja 'utu' wake |
| Hojaji | Orodha ya maswali ya kujibiwa na kundi fulani la watu katika utafiti (kidadisi). |
| Analojia | Hali au tabia ya kitu kufuata mkondo au sura ya kitu kingine kinachotangulia. |

## 1.8 MSINGI WA NADHARIA

Katika utafiti huu, tuliongozwa na Nadharia ya Upole ya Penelope Brown na Stephen Levinson (1987). Kinadharia utafiti huu unahusiana na uwanja wa pragmatiki ambao kwa kawaida huhusika na unenaji na si sentensi. Nadharia ya Upole ilitusaidia kuelezea vile lugha ilivyotumika kama mkakati wa upole katika kuelezea maswala nyeti ya jamii.

### *1.8.1 Nadharia ya Upole*

Wataalamu wengi wameandika kazi zao kulingana na mikakati ya upole, lakini wale ambao mapendekezo yao yametokea kuzama katika Nadharia ya Upole vyema ni Brown na Levinson (1987) ambao walikuwa wanaanthropolojia wa kijamii kule Uingereza. Historia ya Nadharia hii ilipata msukumo kutoka mwaka wa 1963 pale Erving Goffman alipochapisha makala juu ya *'kazi za uso'*. Ndiye aliyeanzisha dhana ya 'uso' ambayo imekuwa kama 'mpigo wa moyo' wa Nadharia ya Upole. Kulingana naye Goffman dhana hii ya 'uso' ilitokea Uchina ambapo Goffman aliikopa na ambayo ilitumika kuashiria hali ambapo mzungumzaji au hata msikilizaji angetaka hali yake katika mtagusano wao idumishwe. Goffman anazungumzia uso kwa kuangazia namna watu wanavyotokea kujibainisha katika mtagusano katika jamii na wanadai kuwa ukweli unajengeka katika maingiliano yetu ya kijamii.

Nadharia hii vile vile imechota mali yake ghafi kutoka kwa kazi yake Leech (1986) inayohusu Kanuni za Upole *(politeness maxims)*. Kanuni hizi nazo zimetokana na kuimarishwa kwa Misimamo ya Ushirikiano yake Grice (1975) *(co-operation principle).*

Msingi wa Nadharia hii unafumbata vitengo muhimu kama vile; *Kuwa kwenye rekodi, Upole chanya, Upole hasi na Kuwa nje ya rekodi.*

Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson imejengeka katika msingi wa kipengee cha uso chake Goffman. Imani iliyo muhimu na matini yao asili ni kuwa, huwa tunabadilisha lugha kutokana na msikilizaji, hivyo basi kuegemea mikakati ya upole kwa kuzingatia hadhira. Kulingana nao Brown na Levinson huwa tunasawiri ujumbe kila siku maishani ili kukinga uso na kufanikiwa katika mambo mengine.

Tishio la uso wa mtu limetokea kujulikana kama Tendo La Kutishia Uso *(FTA).* Brown na Levinson wanadai kuwa Kitendo cha Kutishia uso kinahitaji kuwepo kwa maelezo ya kupunguza makali au uneni wa upole wa kurekebisha, au mazungumzo yatatokea kutoafikiwa. Brown na Levinson wanatanguliza kwa wazo la kuwepo na watu wenye ruwaza nzuri, wanaoweza kuigwa, hawa ni watu ambao wanafikiri kirazini, kwa mikakati, na wana ufahamu wa uchaguzi wao wa lugha. Hawa ni watu ambao ni razini, wenye mikakati mizuri na wanaojali uchaguzi wao wa uneni. Wanakubaliana na mwelekeo wake Goffman wa 'uso', yaani, watu hawa razini wanao Uso Chanya na Hasi. Kwa kawaida watu ambao ni vielelezo vyema hupenda kujali nyuso za wengine lakini hujikuta wametokea kufanya vitendo vya kudhuru nyuso. Mikakati ya upole hukuzwa ili kuelekeza ujumbe unaonuia kuokoa uso wa msikilizaji wakati Tendo la Kutishia Uso haliepukikwi au vinahitajika (Ufafanuzi wake Mills: 2003:12), kimsingi mzungumzaji huepuka kumghasi au kumfanya anayemsikiliza asikose starehe.

*Tendo la kuutishia uso hasi*

Uso hasi hutishiwa wakati mtu haepuki au hatarajii kuzuia tendo la uhuru la mshiriki katika mazungumzo. Tendo hili huenda likamdhuru aidha mzungumzaji au hata msikilizaji na kumfanya mmoja wao kunyenyekea chini ya mwingine. Kwa kawaida uhuru wa uchaguzi na kutenda huzuiwa wakati uso hasi umetishiwa.

*Kudhuriwa kwa msikilizaji*

- Tendo linalokiri au kukana jambo la baadaye la msikilizaji linalomshinikiza msikilizaji kufanya au kutofanya tendo fulani. Kwa mfano*; kulazimisha, kuomba, mapendekezo, ushauri, vitisho n. k.*
- Tendo linalopendekeza maoni au kuwepo kwake msikilizaji kwake mzungumzaji, mfano; *kusifu, maelezo ya kutamani, chuki, hasira,*
- Tendo linaloelezea tendo chanya la baadaye la mzungumzaji kwake msikilizaji ambapo, kwa kufanya hivyo msikilizaji huwa ameshinikizwa kukubali au kukataa tendo au awe mdeni; Mfano; *ahadi au toleo*.

*Kudhuriwa kwa mzungumzaji*

Hili ni tendo linalodhihirisha mzungumzaji anashindwa kukabiliana na shinikizo la msikilizaji, hivyo basi kutokea; *kushukuru, kukubali udhuru, kuomba msamaha, kukubali kuzawadiwa, jibu la msikilizaji baada ya kukiuka maadili ya kijamii n. k.*

Tendo la kutishia uso chanya

Tendo la kuudhuru uso chanya hutokea pale mzungumzaji au msikilizaji hajali hali ya yule wanayeingiliana naye au hata kutotaka yale mwenzake anayataka. Tendo la kuudhuru uso chanya huenda likamwathiri mzungumzaji au hata msikilizaji. Wakati mtu anapotengwa na wengine ili kuzifanya hali za wengine kutodhaminiwa, uso chanya huwa umedhuriwa.

*Kudhuriwa kwa msikilizaji*

Hili ni tendo linaloelezea ukadiriaji hasi wa mzungumzaji kutokana na uso hasi au elementi ya uso hasi wa msikilizaji. Mzungumzaji huenda akadhihirisha kutokukubaliana kwake kwa njia mbili; njia ya kwanza ni pale mzungumzaji anadhihirisha bila kuzunguka au kwa kuzunguka kuwa haziafiki hali fulani za msikilizaji kama vile matakwa yake, au hata tabia zake. Njia ya pili ni pale mzungumzaji anatokea kutoliafiki jambo fulani na kusema waziwazi kuwa jambo fulani ni baya, halina mashiko au msikilizaji hajaelekezwa vizuri; kwa mfano, maelezo ya kukataliwa kama vile (kutukanwa, kulaumiwa, kulalamikiwa) kutoafikiana, ukinzani n k.

Hili ni tendo linaloelezea hali ya mzungumzaji isiyokuwa tofauti na uso chanya wa anayeelezewa.

- Anayeelezewa anaweza kuudhiwa au akamwogopa mzungumzaji (kuwepo na maelezo mengi yenye kuzua mhemko).

- Mzungumzaji anadhihirisha kuwa hana manufaa ya sawa na msikilizaji, au si mwoga kama msikilizaji. Mfano; **kukosa heshima, kuzungumzia mada zisizohusiana na muktadha.**
- Mzungumzaji kudhihirisha kuwa ana uwezo wa kutojali kuvurugwa kwa akili ya msikilizaji. Kwa mfano; **kudunisha, kujinaki.**
- Msikilizaji kudhihirisha kuwa kuna uwezekano wa kutokea kwa tendo la kuudhuru uso. Hili hutokea pale mzungumzaji anazua mada inayozungukia swala nyeti la kijamii, kwa mfano; **maswala yanayozungukia siasa, ubaguzi wa rangi, dini** n. k.
- Mzungumzaji kudhihirisha kuwa hana jambo badalia linaloendana na matarajio ya uso chanya kwa msikilizaji. Hili kwa kawaida hutokea pale ambapo kuna maelezo ya wazi ya kutokuwepo na mwenendo wa ushirikiano, kwa mfano; **kukatana kalima / kauli.**
- Mzungumzaji kumtambulisha msikilizaji kwa njia ya kumkosea au kumuudhi. Hili linaweza kutokea kiajali au pasina kutarajia. Hili kwa kawaida hurejelea matumizi mabaya ya istilahi au maneno yanayoendana na hadhi, jinsia, au umri, kwa mfano; kumtaja mwanamke wa umri mdogo kama, mama badala ya dada.

*Kudhuriwa kwa mzungumzaji*

Tendo linalodhihirisha kuwa mzungumzaji kwa namna fulani amekosea, na ameshindwa kujithibiti.

- Kuomba msamaha; hapa kwa msikilizaji anajidhuru kwa kukiri kuwa alifanya vibaya zamani.

- Kukubali kusifiwa pindi asifiwapo
- Kushindwa kuizuia hali yake ya kimwili
- Kushindwa kuizuia hali yake ya kihisia
- Kujidhalilisha / kujidunisha
- Kutubia mambo fulani aliyofanya zamani

Mikakati ya upole

Mikakati ya Upole hutumika kuelezea jambo kwa utaratibu ili kuuokoa uso wa msikilizaji wakati Tendo la Kutishia Uso halina budi kutokea au hata kama linahitajika. Brown na Levinson waliorodhesha aina nne kuu za mikakati ya upole kama tulivyoelezea awali; Kuwa kwenye Rekodi, Upole Hasi, Upole Chanya na kuwa Nje ya Rekodi.

Kuwa kwenye Rekodi

Mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi kwa kawaida huwa haujaribu kupunguza tishio la uso wa msikilizaji, japo kuna njia ambapo upole wa Kuwa Kwenye Rekodi hutumika ili kujaribu kupunguza uthabiti wa tendo la kutishia uso. Matumizi ya mkakati huu huzua mhemko au maudhi kwa msikilizaji na kwa hivyo mkakati huu kwa kawaida hutumika pale palipo na ukuruba mzuri wa ushirikiano wa mzungumzaji na hadhira, kama vile familia, au hata marafiki wa karibu.

Brown na Levinson walidokeza matukio kadhaa ambapo mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi unaweza ukatumika;

- Hali ambapo kupunguza kwa tishio hakutokei.
- Kuwepo kwa dharura au pasipokuwa na tumaini; mfano, **Jihadhari bwana!**
- Kuzungumza kana kwamba ustadi mkubwa sana unahitajika;

  mfano, **Nisikilize wewe!**
- Kuwepo au kutokuwepo na haja ya kuudumisha uso wa mtu;

  mfano, **Usisahau kumwoshea nguo leo!**
- Pale utekelezaji wa Tendo la Kutishia Uso linamfaidi msikilizaji;

  mfano, **Eh bwana zipu yako...**
- Kumkaribisha mtu; mfano, **Ingia, mlango u wazi.**
- Pendekeza jambo / toa kitu; mfano, **Liache gari hilo nitalipeleka mwenyewe.**

Upole chanya

Mikakati ya upole chanya hudhamiria kupunguza Tishio La Uso Chanya wa msikilizaji. Hutumiwa ili kumfanya msikilizaji aifurahie hali yake, mahitaji yake, au aliyonayo; na wakati mwingi hutumika katika hali ambapo hadhira inafahamiana kwa uzuri. Upole Chanya huhusisha vile vile kuzungukazunguka na kujaribu kuzuia migongano, kuwepo na uneni wa kirafiki, umoja, kupeana sifa; mifano ya Upole Chanya ni kama vile,

- Huzingatia mahitaji ya msikilizaji wake; mfano, **Leo hauna raha, nikusaidie vipi?**
- Mtu kuwa na matumaini mema; mfano, **Nitakuletea kitabu chako kama hautajali.**
- Huhusisha mzungumzaji na msikilizaji katika shughuli fulani.

  Mfano; **ikiwa tutawafunza wanafunzi hawa vyema, matokeo ya mtihani wao huenda yataridhisha.**

- Kutoa kitu au ahadi, kwa mfano; **Ukija kwa nauli yako nitakurejeshea.**
- Kuzidisha au kutia chumvi kwa faida ya msikilizaji. Kwa mfano; **Nguo hiyo inakuchukua, ulizaliwa kwayo?**
- Kuzuia kutoafikiana kwa jambo. Kwa mfano; **chakula chenyewe kizuri kweli, japo chumvi imezidi.**
- Kuzua mzaha katika mazungumzo. Kwa mfano; **Lahaula bwana! Hicho ni chombo kweli.**

Upole hasi

Mikakati ya upole hasi huelekezwa kuelekea uso hasi wa msikilizaji na unashadidia kuzuia kujishinikiza kwa msikilizaji. Mikakati hii hukisia kuwa mzungumzaji atamlazimishia msikilizaji na kupelekea kuwepo na kiwango kikubwa cha kuleta mafadhaiko au hata maudhi zaidi ya mikakati ya kuwa kwenye rekodi na mikakati ya upole chanya. Uso hasi ni uhitaji wa kutaka kusalia huru na ndio mzungumzaji atakuwa mwepesi wa kuwa na njia ya kumhusisha msikilizaji, kwa kujitenga na njia za kuomba udhuru.

Mifano yao Brown na Levinson ni kama vile;

- Usiwe dhahiri; kwa mfano, **Je unajua kitabu changu kilipo?**
- Tumia njia za mzunguko / au maswali; kwa mfano, **huenda labda atakuja kesho au unaweza kunipitishia kalamu hiyo?**
- Bila rajua (kuona kuwa kila kitu ni kibaya); kwa mfano, **hauna njia yoyote ya kumsaidia mtoto yule, itawezekana?**
- Tumia pronauni za wingi; kwa mfano, **wanahofia kuwa hawataruhusiwa tena.**

- Matumizi ya tasifida (matumizi ya maneno ya adabu yaepukayo miiko lugha); kwa mfano, **John ana mkono mrefu** (kumaanisha kuwa ni mwizi)
- Madanganyo ya upole; kwa mfano, **tutazikosa huduma zako, pengo uliloacha ni kubwa.**

Carter na McCarthy (1994) wamekubaliana nao Brown na Levinson katika maelezo yao kuhusiana na Upole Hasi unapoelezewa kama Utafutaji wa Fadhila, au mzungumzaji kuomba msikilizaji fadhila. Huu ni mfano ulio dhahiri wa mikakati hasi ya upole inayotumika. Kuna hatua tatu za utafutaji wa fadhila; Hatua ya matayarisho, Hatua ya kulenga, na Hatua ya mwisho.

Hatua ya matayarisho hudhihirika pale utafutaji wa fadhila unapotanguliwa na maelezo mapana ya tahadhari dhidi ya Tishio la Uso wa pande zote mbili. Kwa kawaida huhusisha ishara za ufunguzi na vipimo vinavyotumiwa kuisawiri hali (kwa mfano, **"ni aje"** **"unaona"** au **"sasa"**). Kwa kawaida ombi huwa laini, na lisilokuwa la moja kwa moja, na lisilolazimishia (mfano; kauli ya wakati uliopita hutumiwa, **"Nilikuwa sifahamu kuwa leo ..."** au hata kuwepo kwa maswali yasiyo dhahiri, **"Utakumbuka vipi tukio ..."** mzungumzaji lazima kuudumisha umuhimu wake na kuuzidisha ule wa msikilizaji.

Hatua ya ulengaji imegawika katika elementi kama vile sababu za muulizaji au vizingiti alivyo navyo (mfano, **Nimejaribu kila mahali lakini sijapata chochote mpaka sasa**) sura nyingine ni kama vile (**wewe ndiye pekee ninaeweza kutegemea**) na zaidi.

Hatua ya tatu ni ile ya mwisho ambayo inajumlisha shukrani za kutazamia, za ahadi na kusifia (**Nilijua hutanitupa wewe ni malaika**)

Nje Ya Rekodi

Mkakati wa mwisho uliodokezwa na Brown na Levinson ni mkakati usiokuwa wa dhahiri. Mkakati huu hutumia njia ya mzunguko na kumfanya mzungumzaji kutolazimishia jambo. Kwa mfano; mzungumzaji anayetumia njia ya mzunguko kwa msikilizaji wake yaweza kuwa hivi, **"kilichoko tumboni mwangu ni ile chai ya jana,"** maelezo yaliyofichwa hapa ni kuwa msemaji anahisi njaa na anauliza kama kuna uwezekano wa kuwepo na chochote cha kula, bila kuuliza waziwazi msikilizaji akaandae chakula.

### *1.8.7 Mahitaji ya uso*

Yule (1996:61) anarejelea dhana ya uso kama '*mahitaji ya uso*' na kusema kuwa watu hufanya mambo wakiwa na matarajio kuwa mitazamo ya umma kuwahusu itaheshimiwa. Kwa kawaida kila mtu atatarajiwa kuheshimu mahitaji ya uso wa mwingine, kwa hivyo kuna njia nyingi za kutekeleza vitendo vya kuokoa uso.

Nadharia hii itatufaa pakubwa kwani jambo la kimsingi ni kuwa mtumiaji wa lugha kila mara huegemea mkakati fulani ili kuunusuru au kuepuka kuudhuru uso wa msikilizaji wake kwa kutegemea kile anachodhamiria kuwasilisha. Mikakati ibuka katika nadharia ndiyo ambayo itaufanikisha utafiti kwani hii ndiyo mihimili ya kutambulisha namna vijana wanavyoitumia lugha yao wanapowasiliana na makundi tofauti.

## 1.9.0 MAPITIO YA MAANDIKO

### *1.9.1 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti*

Lugha ama kwa hakika imefinyangwa kwa njia tofauti ili kutumiwa kama kifaa cha kupitishia ujumbe kuhusiana na maswala tofauti. Ipara na Maina (2008:59) wanasema kuwa makundi tofauti ya wanaoitumia lugha hutokeza na namna mbalimbali ya kuitumia ile lugha moja, hii ina maana kuwa mtu mmoja anaweza kutumia lugha kwa namna tofauti kutegemea jambo analotenda na mahali anapolitendea. Wakiangazia lugha na umri (k h j: 69) wamedai kuwa matumizi ya lugha hutegemea ongezeko la umri wa watu, wazee huwa hawabwagi mambo kama vile vijana wanavyofanya. Lugha ya wazee huonyesha hekima na busara, madai yao ni kuwa vijana hukosa hekima, yaani adimiko la busara husheheni matumizi yao ya lugha. Madai haya yamezua hamasa ya kutaka kuitafiti mikakati ya upole inayotumiwa na vijana katika matumizi yao ya lugha.

Buliba na wenzake (2006:61) wakiangazia lugha na umri wanasema kuwa katika mawasiliano baina ya vijana na wazee, vijana hutumia lugha ya adabu na heshima, vilevile vijana huzua msimbo wao wenyewe. Kutokana na kukinzana kwa msimamo wao Buliba na wenzake (k.h.j) na wao Ipara na Maina (k.h.j) kuna haja kuufanya utafiti huu ili kutokea na kauli yenye mashiko, utafiti wetu unadhamiria kufanya hili.

Njeri (2007:20) akiwanukuu Fromkin na Rodman (1988) anasema kuwa jamii huunda istilahi lugha inapokuwa katika mkondo wa kukua na baadaye kutokea na mipaka ya uamuzi ni yapi ya kusemwa kuashiria upole na yale yasiyo ya kusemwa kiholela. Wanasema

kuwa msamiati wowote ule unamzungukia mwanadamu, lakini muktadha lengwa wa kijamii ndio huamua ni lipi la kusemwa na lisemwe wapi, wanaendelea kusema kuwa, 'uchafu au uzuri wa lugha lazima uwepo kwenye sikio la msikilizaji au katika mtazamo wote wa kijamii.' Kwa sababu vijana ni sehemu muhimu ya jamii, utafiti huu umedhamiriwa kuchunguza mikakati ya upole ya lugha ambayo hutumiwa na vijana katika matumizi ya lugha katika mawasiliano.

Hudson (1995) aliutafiti ushirikiano uliyopo baina ya lugha na jamii na akaibua kuwa kuna njia tofauti ambazo makundi tofauti ya jamii hutumia lugha. Msomi huyu aliibua kuwa lugha kama inavyotumika na makundi tofauti kitabaka hubadilika kama vile hali zao zinavyobadilika kitabaka. Amesema bayana kuwa wafanyi kazi katika sehemu tofauti tofauti hutumia lugha kwa njia iliyo tofauti. Vijana ambao utafiti wetu unalenga ni wa shule za sekondari. Utafiti wetu unatarajia kuchanganua mikakati inayosheheni matumizi yao ya lugha, tena kama sehemu muhimu ya kujitathmini.

Trudgill (2002:58) anasema kuwa katika jamii nyingi, usemi wa wanaume na wanawake hutofautiana. Anashadidia kauli hii kuwa lugha haitofautiani tu kuambatana na tabaka kijamii, kikundi cha kikabila, umri na jinsia ya msemaji lakini vile vile muktadha huchangia. Vijana kama kikundi muhimu katika jamii nacho kina vijana wavulana na vijana wasichana, kwa mantiki hii basi utafiti wetu ulidhamiria kuchanganua tofauti ya mikakati ya upole ya kikundi hiki katika matumizi ya lugha.

Buliba na wenzake (k.h.j: 88) wanasema kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya lugha, jamii na utamaduni kwani tangu jadi katika tamaduni mbalimbali lugha imeonyesha tabia ya kuwa na maneno ambayo licha ya kwamba hayakupigwa marufuku, huruhusiwa kutumiwa katika mazingira fulani tu na watu mahususi. Jamii kwa kawaida hustahi matumizi ya lugha iliyosheheni adabu ambapo azma kuu huwa kuhifadhi na kuhami maadili ya jamii. Miiko lugha mingine hujaribu kuzuia au kuondosha kabisa kitu fulani. Kutokana na maelezo haya ukweli unaibuka kuwa hata vijana kama sehemu ya jamii wana mikakati mahususi ya upole katika matumizi ya lugha ili kuhifadhi na kuhami maadili fulani ya jamii. Utafiti wetu unadhamiria kuichunguza mikakati inayotumiwa na vijana kuhami lugha yao wanapozungumzia maswala nyeti ya jamii.

Rayson na wenzake (1997) alitekeleza uchanganuzi wa kurudiwa kwa vipengele vya msamiati katika komponenti za mazungumzo katika kongoo za kitaifa za Uingereza. Utafiti wao uligundua kuwa wanaume na wazungumzaji chini ya umri wa miaka 35 walitumia miiko lugha yaani lugha isiyokuwa ya upole nalo daraja la kitabaka halikuathiri matumizi ya maneno ya kuapia. Utafiti wake Rayson (k.h.j) ulilenga vijana wa kiingereza. Utafiti wetu unanuia kuangazia vijana wanaotumia lugha ya Kiswahili katika mazingira tofauti katika shughuli zao.

Stenstrom (1999) alichanganua maneno elfu 21,000 ya kongoo ndogo kutoka kwa kongoo yenyewe, na kugawa kwa usawa wanawake na wavulana wa umri wa miaka 16 waliofikiriwa kuwa wa tabaka la katikati juu, na kushirikishwa katika majadiliano ya jinsia moja.

Aling'amua kuwa wasichana hutumia maneno sisitizi kama vile (***kweli, hakika)*** zaidi ya wavulana, lakini walitumia istilahi zilizokuwa zimedhibitiwa zaidi ya wavulana ambao huongezea maneno apizi katika usemi wao uliozidishwa.

Njeri (2007) katika tasnifu yake aliangazia swala la upole katika matumizi ya lugha safidi na ubora wake katika kuwasilishia ujumbe unaohusiana na swala la UKIMWI. Maswala ambayo yaliibuka ni kuwepo na mielekeo tofauti kuhusiana na matumizi ya lugha safidi katika kuwasilisha ujumbe unaohusiana na UKIMWI akiilenga jamii ya Gikuyu. Njeri aliulenga UKIMWI na usimbuaji wa ujumbe ndani ya lugha safidi, yani kama lugha ya upole ilichangia katika kuuwasilishia ujumbe wa UKIMWI. Sisi tunatambua kuwa vijana kama sehemu ya jamii na ukamilifu wake huwasiliana katika maswala mengi sana na kwa sababu mikakati sharti iwepo katika kukamilisha mawasiliano, basi tumeona kuwa kuna haja ya kuitathmini mikakati ambayo vijana hutumia wakati wa kuwasiliana.

Msanjila (2007) katika jarida la *Nordic Journal of African Studies* aliangazia utumiaji wa Kiswahili na lugha za Jamii kijinsia nchini Tanzania katika vijiji vya asili ambavyo viko mbali na miji, matokeo yake yalikuwa, wanawake chini ya walio na umri wa miaka 35 walitokea kukitumia Kiswahili zaidi. Msanjila (k.h.j), akimnukuu Tripp (1969) anasema kuwa wanawake wanapenda kutumia lugha ya upole kuliko wavulana ambao wao hupendelea kutumia lugha ya ujasili na ya kujiamini; Utafiti wetu umedhamiria kujikita katika mikakati ya upole ya matumizi ya lugha ya vijana, jambo hili halijashughulikiwa.

Wambua (2009) katika tasnifu yake ameangazia swala la miiko lugha na lugha safidi ambapo alichunguza tofauti ya lahaja na mielekeo kuhusu maneno miiko na maneno safidi ya Kikamba. Aliangazia kama tofauti ya kijamii inayoendana na jinsia, umri, na tofauti za kilahaja vile zinaathiri mielekeo ya watu, na kuradidi kwa uchaguzi wa maneno safidi. Tafiti zote hizi ziliangazia utafiti kwa kuegemea Kiingereza kinyume na mwelekeo wetu ambao unailenga lugha ya Kiswahili na kudhamiria kutafiti mikakati ya vijana ya upole ya matumizi ya lugha. Kauli yetu inapata mashiko kwani Igboanusi (2001) akimnukuu mwandishi mmoja wa Nigeria anasema kuwa, 'ni lugha ambayo huongoza mwelekeo'. Kuna haja ya kujua kama ni lugha ambayo huongoza mwelekeo wa vijana pale wanapotokea na mikakati ya upole katika matumizi yao ya lugha au la.

Mbaya (2000) katika jarida la *Nordic African Studies* aliangazia matumizi ya miiko lugha katika muktadha wa ndoa; *Languu*, katika kabila la Oromo. Anasema ili kuwepo na mlahaka mzuri kati ya mume, mke na wakwe mbinu badalia huibuliwa ili kufidia mtagusano baina yao. Ikiwa swala la ndoa na matumizi ya lugha safidi limeshughulikiwa kwingineko, mikakati ya upole ya vijana katika matumizi ya lugha linakuwa na manufaa.

Kwa kuangazia kazi tofauti tofauti kama vile ambavyo imedhihirika, ni wazi kusema kuwa kuna pengo kubwa kuhusiana na vile vijana wanavyoitumia lugha yao wanapowasiliana na makundi tofauti katika jamii; tukio hili linatokea kudhihirisha haja ya kuitambulisha mikakati inayotumiwa na vijana.

## 1.10 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii inahusika na uchaguzi wa watafitiwa, utaratibu wa ukusanyaji wa data, vifaa vya ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

### *1.10.1 Uteuzi wa watafitiwa*

Data ilikusanywa kwa kuchagua watafitiwa ambao ni wa shule za sekondari katika eneo la mji wa Nakuru. Uteuzi wa watafitiwa ulitekelezwa kwa mtindo shelabela. Wanafunzi 30 kutoka kwa shule tatu katika Manispaa ya mji wa Nakuru walitafitiwa. Wavulana kumi na watano na idadi kama hiyo ya wasichana ilihusishwa.

### *1.10.2 Ukusanyaji wa data*

Mbinu za ukusanyaji wa data zilihusisha utumizi wa hojaji ambapo watafitiwa walitakiwa kuutumia usemi halisi katika kuzijaza hojaji. Kabla ya kuafikia uamuzi huo majaribio ya utafiti yalifanywa ili kutupa dira katika utafiti wetu. Baada ya hojaji za kwanza kujazwa mtafiti alitambua kwamba kulikuwa na haja ya kuwaelekeza watafitiwa kwani walikuwa wakiyajibu maswali kwa usemi taarifa ilhali walitakiwa kutumia usemi halisi. Baada ya kuitathmini hojaji tuligundua kuwa maswali matatu yalibainisha kuwa tulikuwa tumechukua mwelekeo, hivyo basi ikatulazimu kuyabatilisha kabla ya kuufanya utafiti kamili.

### *1.10. 3 Vifaa vya ukusanyaji wa data*

Kifaa kifwatacho kilitumiwa katika ukusanyaji wa data kuhusiana na maswala ya utafiti.

- Hojaji

### *1.10.4 Uchanganuzi wa data*

Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya maelezo, hii ilipatikana baada ya kuangalia namna watafitiwa walikuwa wamejielezea kwenye hojaji. Matokeo yetu yalitolewa kwa kuegemea tofauti kulingana na asilimia katika kila mkakati ambao ulitumiwa na vijana. Kabla ya kutoa maelezo kwa asilimia ilitubidi kubainisha kila mkakati kwa kutumia nambari ambazo zimedokezwa katika ufunguo katika sura ya tatu. Mikakati hiyo ni kama vile inavyojitokeza katika Nadharia ya Upole.

### *1.10.5* HITIMISHO

Katika sura hii tumeweza kuangazia mada yetu ya utafiti ambayo ni '*mikakati ya upole ya lugha katika matumizi ya lugha ya vijana'.* Tumepiga hatua na kuelezea sababu na umuhimu wa kuichagua mada hii na vile vile, tumeweza kuangazia kazi zingine zinazoizungumzia mada ya utafiti pamwe na hayo, tumeweza kuelezea nadharia iliyotuongoza katika utafiti, hatimaye tumeweza kuelezea ni akina nani walihusishwa kwenye utafiti huu na vile data ilivyokusanywa na hatimaye ilivyochanganuliwa. Kwa kifupi sura hii imeweza kuweka msingi kwa sura zinazofuatia ili kuliwezesha somo la utafiti kueleweka.

# SURA YA PILI

## MAELEZO YA LUGHA KUHUSIANA NA MIKAKATI YA UPOLE KATIKA MATUMIZI YA LUGHA

### 2.1 Utangulizi

Bila shaka lugha ni kifaa muhimu; sio tu kama njia ya kuwasilisha mawazo na elimu lakini pia kuujenga urafiki, utangamano wa kitamaduni na kiuchumi kwa washiriki katika maongezi. Katika historia yote ya mwanadamu, watu wengi wameangazia umuhimu wa lugha. Lugha huelekeza mawazo na hisia kwa kubainisha kwa yakini mtazamo wa mtu.

Lugha hutokea kutumiwa kwa njia tofauti ili kufanikisha mawasiliano. Mawasiliano huenda yakaegemea lugha ya kitamathali, lugha ya mzunguko, lugha na utamaduni, uchanganyaji / uhamishaji wa misimbo, uchaguzi wa msamiati, lugha na uhusishaji n.k
Sura hii inadhamiria kuangazia sehemu hizi kwani mikakati ya upole ya vijana ya matumizi ya lugha hutokea kuegemea maswala kama haya wakati wanapoitumia lugha.

### 2.2 LUGHA YA KITAMATHALI

Lugha ya kitamathali hurejelea maneno, na makundi ya maneno, ambayo hutia chumvi au kubadilisha maana ya kawaida ya sehemu ya maneno. Lugha ya kitamathali inaweza kuhusisha analojia ya dhana zilizofanana, au miktadha mingine, na inaweza kuhusisha kutia chumvi. Kubadilisha huku ndiko kunakopelekea kuwepo kwa *tamathali za usemi.* TUKI (1990:26), '...hii ni mbinu ya kupanua maana ya neno (au maneno) ili kupata athari fulani

iliyokusudiwa, mfano... *Yule golikipa ni nyani yule!* Neno nyani limetumiwa kuonyesha uhodari wa golikipa katika kudaka mpira'

Wamitila (2003a:102) anasema, 'hii ni dhana inayotumiwa kuelezea lugha ambayo sio ya moja kwa moja, lugha tamathali huwa na sifa za kisitiari au huwa na sifa fulani za kibalagha.'

Katika lugha ya kitamathali misemo ya kimatilaba huongezea vidato vya kimaana katika matumizi fulani ya lugha. Ili kuubadilisha usemi, ubongo wa mwanadamu huhitaji kiunzi tambuzi kinachohusisha kumbukumbu ambazo huenda zikawa ndizo maana ya neno la kuegemewa katika muktadha fulani. Seti hii ya kumbukumbu itadokeza kwa yakini maana iliyo wazi au ya kimatilaba, vilevile inaweza kupendekeza sababu za kuashiria maana tofauti, mfano; msomaji ataelewa kuwa mwandishi au mtunzi alidhamiria kumaanisha kitu tofauti.

Kwa mfano sentensi kama, '*ardhi ina kiu*,' sehemu moja ni ya kitamathali. Ardhi ina maana iliyo wazi, lakini ardhi si hai na kwa hivyo haina kiu na haihitaji kunywa maji. Msomaji kwa kawaida atatokea kutoichukulia maana hiyo iliyo wazi na bila wasiwasi atasimbua maana ya maneno hayo kumaanisha, '*ardhi ni kavu*' analojia hii huenda ikaibua uwezekano wa kuwa wanyama wana kiu. Hata hivyo maelezo, '*Nilipomwona mara ya kwanza, roho yangu ilitetemeka,*' ina ugumu wa kusimbuliwa; Inaweza kumaanisha kupumbazwa, hofu, au jambo jingine tofauti. Ili mtu aweza kusimbua hali iwayo yoyote ile, itautegemea muktadha wa mzungumzaji. Wengine watatokea na maneno machache yenye maana ya muda, lakini

hawataelewa usemi wa kitamathali mpaka pale watakapopata maelezo zaidi. Lugha ya kitamathali inatengana na maana iliyo wazi ili kupata athari maalum au maana.

## 2.3 MTAZAMO WA GRICE WA UHUSISHAJI

Nadharia ya pili ya Grice (1975) ya **uhusishaji** inajulikana vile vile kama **kanuni ya kushirikiana**. Kulingana na Grice ni kuwa, ni lazima mtu achangie jambo katika maongezi kulingana na mahitaji yake, katika hatua linapojia, kwa nia inayokubalika au kuelekea maongezi unayohusika nayo Grice (k.h.j: 26). Kwa kifupi kanuni ya kushirikiana inasema: ***Changia kile kinachohitajika kwa kuegemea nia ya mazungumzo legwa.*** Nadharia ya Grice inaongozwa na 'kanuni nne' zinazoangazia jinsi ya kudhihirisha ushirikiano. Anayoyasema ni mambo yaliyo wazi ambayo watu huyafuata ili kufanikisha mawasiliano.

Kanuni hizi nne ni:

- Kanuni ya ubora.
- Kanuni ya idadi
- Kanuni ya maelezo
- Kanuni ya mtindo

Mtazamo wa Grice kuhusiana na sheria hizi si za mapatano ya kiholela lakini kama mfano wa sheria za kijumla zinazoongoza ushirikiano razini katika mtagusano wa maongezi.

*a) Kanuni ya ubora*

Maelezo ya mkakati huu ni kuwa:

- Jaribu kuufanya mchango wako katika maongezi kuwa wa ukweli.

- Usijaribu kusema mambo ambayo unajua kuwa ni ya uwongo.
- Usiseme mambo ambayo hauna hakika nayo.

Kanuni hii imezifumbata zile zingine zote kwani inachukulia kuwa tunayoyasema tuna imani kuwa ni ya kweli. Kudanganya ni kukiuka kanuni hii kwa mfano; usemi kama huu ni wa uwongo, *'Ukimwi ni homa'*

*b) Kanuni ya idadi*

Maelezo ya mkakati huu ni kuwa:

- Mzungumzaji aufanye mchango wake ueleweke kwa ukamilifu unaohitajika (kwa nia ya mazungumzo ya wakati huo).
- Mzungumzaji asizidishe mchango wake zaidi ya vile inavyohitajika.

Kama inavyodhihirika kanuni hii inahusika na idadi ya yale anayosema mtu kwa majadiliano yoyote. Kanuni hii inatarajia kuwa mchango wa mzungumzaji hautazidi au kuwa chini wa yanayotarajiwa. Kwa mfano tangazo kama hili ***'Tumechill'*** la kibiashara kuhusiana na UKIMWI halitoshelezi kuzua vita vilivyo kamilifu kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

*c) Kanuni ya maelezo*

Kanuni hii vile vile hurejelewa kama kanuni ya uhusiano ambapo maelezo yake ni:

- Kuwa na hakika.

Kanuni hii inatuelekeza kuwa uneni wetu unastahili kupangwa kwa njia ambayo itahakikisha kuwepo na ushirikiano katika mazungumzo.

*d) Kanuni ya mtindo*

Kanuni hii inaeleza kuwa:

- Kuna haja ya kuwa dhahiri.
- Mzungumzaji asitumie maelezo yaliyo na mafumbo.
- Mzungumzji asiyaruhusu maneno yenye utata.
- Mzungumzaji atoe maelezo mafupi. (Toa maelezo yasiyochosha).
- Mzungumzaji awe na utaratibu katika maongezi yake.

Kanuni hii inapendekeza kuwa kuna haja ya kutolea maelezo ambayo msikilizaji atayaelewa vyema na kwa urahisi. Hata hivyo mpango huu huwapoteza watu wakati wametokwa na makini na kukata tamaa, tena kutozingatia kanuni hii hupelekea nguvu ya kuhisi idhihirike. Njeri (2007:18), akimnukuu Gachanja (2005: 62); anasema kuwa Kukiuka mojawapo au orodha ya kanuni hizi huchangia ukamba au sehemu ya mawasiliano kuwa dhaifu.

### 2.3.1 *Uhusishaji*

Dhana ya uhusishaji imechanganuliwa katika Nadharia ya Grice, na kulingana na Kamusi ya Falsafa ya Staford (2005:44), uhusishaji ni jambo lililomaanishwa, lililoangaziwa, lililopendekezwa na dhahiri kinyume na yaliyosemwa. Nadharia ya pili ya Grice ya uhusishaji aliyoiasisi kwa yakini ni nadharia inayohusu vile watu huitumia lugha. Mapendekezo yake ni kuwa kuna seti ya dhana inayozidi na kuongoza utekelezaji wa mazungumzo. Haya huongozwa na kanuni nne za mazungumzo kama vile tulivyokwisha kuangazia. Uhusishaji unadokeza vile mawasiliano yanavyoweza yakaafikiwa pale ambapo pana upungufu wa njia

za makubaliano katika kuelezea ujumbe unaohitajika. Njeri (k.h.j: 19) anasema kuwa mengi huwasilishwa zaidi kulingana na vile yanavyodhihirika katika usemi. Katika mfano wake, akiangazia mazungumzo ya *ukimwi* kuhusiana na Gikuyu; istilahi ***kobokobo*** 'buti ya mpira' au ***mucinga*** 'bunduki' inaleta mahusisho tofauti kinyume na maana ya makubaliano. Kuna jambo ambalo linaangaziwa hapa kuwa kondomu na buti ya mpira vinalenga kitu kimoja; kuwa ni vifaa vya kuzuia maambukizo ya magonjwa ya zinaa.

a) *Kanuni za busara*

Kulingana na imani za kanuni za busara ni kuwa mzungumzaji lazima:

'*Apunguze wazo la imani linalomaanisha gharama kwa mtu mwingine na azidishe wazo la imani linalomaanisha faida kwa mtu mwingine.*' Kwa kufanya hivyo mzungumzaji anadhihirisha upole. Kanuni ya busara inaegemea mawazo ya Searl (1977) ya mapendekezo ya kiutendaji ya ilokusheni inayorejelea kauli ya muktadha wa mtu fulani, matendo mengine yatekelezwe kwa pamoja na msikilizaji na mzungumzaji. Kanuni hii inamaanisha kuwa uneni unaweza kuwekwa katika kipimo cha faida na gharama. Jinsi gharama ilivyo juu ya faida, hivyo ndivyo ufinyu wa upole ulivyo katika uneni, ikiwa kiwango cha gharama kiko chini ya faida hili hudhihirisha wingi wa upole katika uneni.

Leech (1983:105) aliangazia kuwa kanuni ya busara hujumlisha mambo tofauti na viwango tofauti vya upole katika hali tofauti kwa kutegemea majukumu ya matendo anayotenda kama vile kuomba msamaha, kusihi, kukashifu, kuonya n.k. Majukumu ya matendo haya yameorodheshwa katika hali ambapo yanaweza kuwa

shindani, kunjufu, dhibitishi au hata ya migongano; kati ya majukumu haya; mawili ya kwanza ndiyo yanayohusisha upole. Pale majukumu ya matendo ni shindani, upole unatokea kuwa hasi na pale ambapo ni kunjufu, upole unatokea kuwa chanya.

## 2.4. KUCHANGANYA NA KUHAMISHA NDIMI

Dhana ya ubadilishaji na uchanganyaji msimbo au ndimi ni tofauti kwani ubadilishaji huhusiana na kuitumia lugha moja kwa muda na kuiendea ya pili baada ya muda ilhali uchanganyaji huhusiana na kuzitumia lugha mbili au zaidi kwa wakati mmoja. Hali zote hata hivyo hutokana na umilisi wa lugha mbili au zaidi walionao wazungumzaji.

### 2.4.1 Kuchanganya ndimi au msimbo

Ipara na Maina (2008:78) wanasema kuwa kuchanganya ndimi au msimbo ni hali ambapo wazungumzaji wanazungumza kwa lugha moja kisha hapa na pale, wakatoka kidogo katika lugha hiyo na kuingilia lugha ya pili au ya tatu kwa muda mfupi na kisha kurejelea lugha ya awali. Kila mtu ambaye huongea, amejifunza kuhamisha ndimi kwa kutegemea hali na mahali alipo. Katika muktadha wa usomi kuchanganya ndimi kunaelezewa kama mazoea ya kuhamisha lugha baina ya lugha ya msingi na ile ya pili.

Buliba na wenzake (2006: 73) wanasema uchanganyaji msimbo ni hali ya msemaji kutumia vipashio au maneno ya lugha mbali mbali katika hali moja ya mazungumzo. Kwa mfano, msemaji anaweza kuchanganya Kiswahili na Kiingereza hivi:

*By the way,* ulifika lini? Siku*notice.*

### 2.4.2 Kuhamisha ndimi au msimbo

Buliba na wenzake (k.h.j: 71) wanasema ubadilishaji msimbo ni ile hali ya kubadilisha lugha wakati wa mawasiliano. Wanashikilia kuwa hili hutokea pale ambapo msemaji wa lugha ana umilisi wa zaidi ya lugha moja. Msemaji huweza kubadilisha mazungumzo yake kutoka lugha moja hadi nyingine anapotokea kuathiriwa na hali iliyopo na mtindo; kimsingi hali hii hutegemea washiriki, mada na mandhari. Madhumuni ya kubadilisha msimbo hutokana na haja ya mzungumzaji kusisitiza kile anachosema. Inawezekana vile vile kubadilisha huku kukafanywa ili kudhihirisha hisia fulani. Wazungumzaji huenda wakatumia Kiswahili pamwe na Kiingereza. Kwa mfano,

*Imagine I can't wait anymore.*

### 2.4.3 Tasifida kama msimbo

Kujadili mambo ya siri kunaweza kuafikiwa kwa kuelewa tasifida zinazoeleweka na wachache. Vijana wakati mwingine huisafidi lugha wanapozungumzia maswala yenye kuzua mihemko, hata kama watu wengine wako karibu. Vijana hubuni maneno misimbo na istilahi ili kuwasiliana kisiri hata kama kuna watu wengine.

Tasifida nyingi zinazotumiwa na vijana zinachotwa kutoka kwa matukio ya kila siku katika mazungumzo au katika kundi jamii fulani. Chimbuko la misimbo ili kuisafidi lugha hutokana na jamii na mandhari anapojipata mwanadamu, ukopaji kutoka kwa lugha za kigeni na marejeleo ya Bibilia. Maonyo ya Bibilia ni wazi kuhusiana na lugha chafu; katika Kitabu cha Waefeso 4.29 Paulo anazungumzia swala la matumizi ya lugha tunayoitumia, '*neno lolote*

*lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kulihitaji, ili liwape neema wanaosikia. '*

Katika jarida la *Nordic Journal of African Studies* 16(3): 320 - 332 (2007) katika makala ya Lugha Kama Kitambulisho: Changamoto ya *Sheng* Nchini Kenya, King'ei na Kobia wanayaafiki mawazo ya Ogechi (2005) kuwa uundaji wa maneno katika msimbo huu hutumia njia mbali mbali. Msimbo huu hupelekea kuibuka kwa matumizi ya jazanda na maneno ya tasifida. Ukweli unaoibuka katika hali hii ni kuwa vijana na watumiajii wengine wa *Sheng* hutaka kudhihirisha upole katika maswala ambayo kwa kawaida huzua mtafaruku maswala ya kukirihisha yanapotokea kuzungumziwa.

Kwa mfano;

- Boli humaanisha mjamzito
- Mahewa humaanisha muziki
- Kuro humaanisha kahaba

Misimbo mingine huenda ikatokana na hali inayoendana na tukio fulani kama vile la onomatopeya, vitendo vya kukirihisha kama vile vya kunya na kukojoa huhusiana na hali za utotoni. Kwa mfano;

- Pupuu humaanisha kwenda haja kubwa
- Susuu humaanisha kwenda haja ndogo n. k

## 2.5 UCHAGUZI WA KILEKSIKA

Katika mawasiliano uchaguzi wa maneno ili kutosheleza mwelekeo alionao mzungumzaji unaweza kuibua utata sana. Nirenburg na Nirenburg (1988) waliangazia swala hili waliposema mtu ambaye ni wa jinsia ya kiume kati ya miaka 13-15 anaweza akawa mvulana, mtoto kijana, mtoto, mvulana wa shule, mzee kijana, au mwanamume. Ili kuchagua neno lolote hapa kutosheleza mahitaji ya muktadha, kuna uwezekano wa kuzuka 'giza'. Marcus (1987), ameangazia kuwa uchaguzi wa kileksika haujazungumziwa sana na wanasarufi zalishi, McDonald (1991) kati ya wengine amelalamika kuwa utafiti wa swala la uchaguzi wa kileksika umevutia jamii ndogo ya watafiti.

Kwa nini uchaguzi wa kileksika kuwa mgumu? Kama vile kuelezea dhana ya kitu kama kihusishi cha kishazi au kivumishi kulivyo na ugumu, kwa kawaida uchaguzi wa neno husawiri uhusiano tofauti na kile kinachorejelewa hivyo basi maana huenda ikabadilika kabisa.

Katika sentensi zingine neno mvulana likibadilishwa na neno lingine kati ya yale tuliyotaja, huenda likaibua maana tofauti. Ili kusuluhisha shida ya uchaguzi, kwanza kuna haja ya kutambulisha tofauti ya visawe kulingana na vile vinavyojitokeza katika leksika na kuzingatia kuwa utaratibu wa uchaguzi huo unadhihirika bayana.

### 2.5.1 Utaratibu wa uchaguzi wa neno

Kumefanywa mchango finyu wa utafiti kuhusiana na utaratibu wa uchaguzi wa neno; kulingana na Hovy's (1988) mwanasarufi zalishi PAULINE katika uchaguzi wake wa vipengee vya kileksika aliuegemea mtazamo wa pragmatiki katika hali husika. (Matarajio ya usemi wa mzungumzaji ambayo huibua mbinu ya malengo, ambapo hili hupelekea uchaguzi fulani wa kileksika). Vile vile akiangazia kiwango cha pragmatiki Elhadad (1991) alisema msukumo alio nao mzungumzaji katika dhamira ya majadiliano yake ndiyo yanayopelekea uchaguzi wa vivumishi. Wanner na Bateman (1990) waliuona uchaguzi wa kileksika kutoka mtazamo hali huru. Uchaguzi huu wa msamiati kwa kiwango kikubwa huegemea mada, muktadha, hadhira, umri, hali n.k.

## 2.6 MAZUNGUMZO YA MZUNGUKO

Kuzungumza kwa njia ya mzunguko kuna majukumu mengi katika mawasiliano; hujaribu kupunguza migongano, kuingiza hila katika habari, kuingiza mzaha katika maongezi, kutoeleza kikamilifu, (kutosema ukweli). Kwa kawaida msikilizaji huenda akamwelewa mzungumzaji hata kama hayaelezei mambo moja kwa moja.

Kanuni za kushirikiana zake Grice (1975) hudokeza namna mtu huweza kuusimbua ujumbe kulingana na vile wengine wanavyosema. Ili msikilazaji aweze kuisimbua habari ya mzungumzaji vyema, msikilizaji huenda akaegemea mtazamo wake Grice ambao aliuita kanuni za majadiliano, na ambao uliangaziwa upya na Levinson (1983) ambapo ametokea kuuangazia kwa misingi ya:

- Kanuni ya ushirikiano.
- Kanuni ya ukweli.
- Kanuni ya idadi.
- Kanuni ya uhusiano.
- Kanuni ya mtindo

*Kwa* kifupi kanuni hizi hudokeza namna washiriki katika mazungumzo wanaweza kujadiliana kwa kuegemea kanuni kisawasawa, kirazini na kwa njia ya kushirikiana; wazungumze kwa kuegemea ukweli, kwa kuegemea uhusiano wa kile kinachosemwa na kwa njia ya wazi ili kuitoa habari toshelevu(Levinson k.h.j 102- 3).

### 2.6.1 Nadharia ya Uso

Nadharia ya Uso ya Ervin Goffman inaelezea kwa yakini ni kwa nini watu husema mambo kwa njia ya mzunguko; ni kwa msingi huu wa nadharia ambapo Brown na Levinson(1987) walitokea na maelezo kuhusiana na Nadharia ya Upole.*(international communication studies 111:1 1993:64)*

### 2.6.2 Ujumbe unaowasilishwa

Kulingana na Tannen (1984) aliiasisi Nadharia ya mbinu ya majadiliano kwa kuitumia Nadharia ya Upole ya Lakoff. Tannen aliangazia sheria za Lakoff za upole kuwa zilihusisha kanuni tatu ambazo ni:

i)Usilazimishe (umbali)

ii)Toa nafasi ya uchaguzi (tofautisha)

iii)Dhihirisha urafiki(udugu)

Tannen anasema kuwa uchaguzi wa kanuni yoyote ile hupelekea kuibuka kwa mbinu ambayo itaegemea matukio kama yale ambayo yamedokezwa kwenye mabano. Sheria ya kwanza inasawiri picha ya kuwepo na umbali baina ya mzungumzaji na msikilizaji hivi kwamba kulazimisha hakupo. Ili kuuweka umbali (masafa) kutoka kwa wengine; anasema kuwa maelezo ya kawaida hutumiwa au matumizi ya msamiati wa kudhihirisha ufundi hupewa kipaumbele ili kupunguza nafasi ya msikilizaji kuingiwa na mhemko. Kulingana na Brown na Levinson sheria hii inawiana na mkakati wao wa Upole Hasi. Kanuni ya pili, kutofautisha kunahusiana na kuyasema mambo waziwazi au kwa kuyatumia maneno safidi.

Sehemu hii huhusisha tofauti ya kihadhi baina ya mzungumzaji na msikilizaji ambapo mzungumzaji huegemea kwenye matakwa ya msikilizaji kwa kumwachia msikilizaji kuamua msimamo wake. Kulingana na Tannen, wanawake ndio ambao wana sifa hii ili kuonyesha unyenyekevu wao kwa wengine au huwaachia wasikilizaji wao maamuzi. Mkakati huu unaendana na ule wa Brown na Levinson wa Upole Hasi na unahusisha kuelezea mambo kwa njia ambayo si ya moja kwa moja, yaani ya mzunguko.

Kanuni ya tatu, yaani udugu, kwa upande mwingine kuna msisitizo wa usawa kati ya mzungumzaji na msikilizaji ambapo tendo hili hupelekea kuwepo kwa uhusiano bora kati ya wahusika. Kwa kuegemea kanuni hii, mkakati wa Upole Chanya wa Brown na Levinson baina ya mzungumzaji na msikilizaji unadhihirika. Katika kanuni hii, tukio la kuelezea jambo

kwa njia ya mzunguko linadhihirika kwani wahusika wanatokea kufahamiana vyema, hivyo basi hamna haja kuzungumza, kwa sababu hii basi, njia ya mzunguko bila shaka itatokea kuleta maelewano baina ya wahusika.

Kwa kuitumia Nadharia ya Lakoff ya upole kama msingi wa uchaguzi wake, Tannen (1989) anaelezea majukumu ya njia za mzunguko katika mawasiliano kama:

> Umuhimu wa sura ya lugha ndio uchanganuzi wa maandishi huuita umbo nao uchanganuzi wa majadiliano huyaita mazungumzo ya mzunguko (au katika maelezo ya kawaida ya pragmatiki, hujulikana kama uhusiano): kuuwasilisha ujumbe ambao haujasemwa. (Tannen 1989:23) TY.

Tannen anazidi kusema kuwa mazungumzo ya mzunguko daima yapo na hayawezi yakaepukwa katika mtagusano wa majadiliano. Ameelezea umuhimu wa maelezo ya mzunguko katika majadiliano kwa kuitumia Nadharia ya Lakoff na kuioanisha na yao Brown na Levinson:

> Lakoff (1973, 1979) anazielezea na kuzitalii njia ambazo kwa kawaida wazungumzaji hawamaanishi kwa yakini wanayosema. Maelezo ya mzunguko kwa kawaida yanashtahiwa kwa ajili ya sababu mbili kuu; kuuokoa uso kama mchango ili kuipa hisi ya maelewano inayopatikana kwa kueleweka bila kusema kile mzungumzaji anachokimaanisha. Zaidi ya hayo, mzungumzaji anapodhamiria msikilizaji au msomaji ajijazie maana fulani katika maelezo fulani, njia ya mzunguko

hupelekea kumshirikisha msikilizaji au msomaji, hivyo kuwepo kwa maelewano ya pande mbili.

### 2.6.3 Majukumu ya mazungumzo ya mzunguko katika mawasiliano

Majukumu ya mazungumzo ya mzunguko katika mawasiliano hutokea kudhihirika kwa njia kadha wa kadha, kama vile; kukiukwa kwa kanuni za Grice za kushirikiana, ubabe na umoja na kutumia mzaha kama maelezo ya mzunguko.

### 2.6.4 Kukiukwa kwa kanuni za Grice za kushirikiana

Wakati watu wanawasiliana kwa kawaida, huenda kanuni za kushirikiana zikakosa kuzingatiwa kwani mtoaji wa habari huenda akahofia kuitoa ikiwa itaudhuru uso wa mwingine. Hili huenda likadhihirika ikiwa msemaji ataulizwa habari juu ya mambo ambayo hataki kusema, uso wake huwa umetishiwa, na hivyo huwa si rahisi kwake kusema ukweli na kwa hivyo kanuni za Grice hukiukwa.

Brown na Levinson (1978:213-229) wameelezea njia za kufanya Tendo La Kutishia uso kwa njia ya mzunguko: kanuni ya uhusiano isipozingatiwa basi mtu hutokea kuitumia njia ya mzunguko kwa kutolea maelezo mafupi mafupi na wakati mwingine kwa kutumia ishara za vihusishi. Kanuni ya ukweli hukiukwa mtu anapotumia maelezo ya kukipa kitu / mtu fulani sifa kuzidi au chini ya ukweli, ili kufidia hali hii; kwa mfano, mtu hupapatia mahali fulani sifa isiyostahiki; mtu mwizi huenda akaitwa malaika katika hali nyingine. Kanuni ya idadi inapokiukwa mzungumzaji huenda akaifidia hali hii kwa kutumia sitiari, chuku n.k. kwa mfano, mahali ambapo panavunda huenda pakaambiwa panavutia sana.

### 2.6.5 Ubabe na umoja

Hili linaendana na vile watu wanavyohusika katika mambo fulani na uhitaji wa uhuru wao katika maisha. Ubabe unahusiana na namna mtu huweza kumumiliki mtu mwingine - na kuhusika hata zaidi - na kukataa kutawaliwa na mtu mwingine - na kuzidisha uhuru; haja ya kutotaka kulazimishwa kufanya jambo.

Katika maisha, ubabe hujizingizia kama hali ya kuleta umoja. Mfano mzuri ni pale baba mzazi anapotoa masharti kwa njia ya mzunguko kwa kumwambia binti yake kuwa hataki atoke nje usiku kwa kuifanya hali yake idhihirike kama si ya lazima; yaani kuutumia ujanja ambapo mtagusano katika maisha yetu katika jamii unakuwa shwari.

### 2.6.6 Mzaha kama maelezo ya mzunguko.

Mzaha hutumiwa kwa kusudi la kuchangia kuwepo kwa udugu hasa katika nchi za magharibi. Mzaha katika mwanzo wa mazungumzo huleta ukuruba baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Brown na Levinson (1978:124) wanasema kuwa, "mzaha ni mbinu ya kimsingi katika mkakati wa Upole Chanya." Katika lugha ya Kiswahili mzaha hutumiwa ili kupelekea watu kuona kuwa wanashirikishwa katika hali fulani na kuuhifadhi Uso Chanya wa watu wengine.

## 2.7 LUGHA NA UTAMADUNI KAMA DIRA

Lugha na utamaduni ni reale kwa ya pili, haiwezekani kuuweleza utamaduni pasina kuihusisha lugha; kwa mantiki hii, utamaduni ni tukio la matumizi ya lugha mahyuni (2008).

Lugha imeyafumbata maswala mengi ya jamii na utamaduni, kwa misingi hii itakuwa ni kukosa dira kwa mtu yeyote kuzungumzia lugha na kutokea kutouzungumzia utamaduni.

Buliba na wenzake (2006:20) wanasema kwamba swala la lugha na utamaduni limetazamwa na wataalamu katika njia mbili. Kwanza, kuna wanaochukulia lugha kama chombo muhimu cha kuelezea na kuendeleza utamaduni wa jamii yoyote ile. Pili, kuna wale ambao wanaiona lugha kama sehemu ya utamaduni wa jamii. Lugha ndiyo inayotuonyesha jamii ni nini, inaelezea watu wanaowasiliana wakitumia lugha hiyo. Imedokezwa kuwa mambo muhimu kuhusu maisha ya jamii ya mtoto hupitishwa kwake kupitia kwa lugha, kwa njia hii, mtoto hujifunza utamaduni wa jamii yake, falsafa, itikadi na mambo muhimu yanayodhaminika na jamii yake. Jambo hili linafanikishwa kupitia kwa maingiliano yake na wenzake, na matumizi ya lugha ya kawaida akiwa nyumbani. Katika misingi hii, inakuwa ni vigumu sana kuitenganisha lugha na utamaduni; kwani lugha na utamaduni ni reale kwa ya pili. Buliba (k.h.j: 88) wamesema kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya lugha, jamii na utamaduni.

Upole ni kipengele muhimu cha ishara kinachoendana na mtagusano katika maisha yetu ya kila siku, kwani tamaduni zinadhamini matumizi ya upole katika lugha, Brown na Levinson (1978). Kwa kawaida, linalohusisha udhihirishaji wa upole ili kuuokoa uso, huwa tofauti kutoka kwa utamaduni mmoja na mwingine Eastman (1990), upole ni tendo ambalo limeenea kote katika tamaduni Mahyuni (2008:117). Ni tendo ambalo limeenea kote kwani binadamu katika kila utamaduni hutokea kuwa na mgawo mpana wa matumizi ya lugha ya

upole katika mawasiliano; kwa kifupi matumizi ya upole katika lugha ni elementi yenye mashiko katika mawasiliano baina ya wahusika katika tamaduni zote.

Lugha hutumika na jamii kufafanua imani, itikadi, siasa, uchumi na mifumo yote ya jamii husika. Utamaduni ni mkusanyiko wa fikra na falsafa za watu, ada, desturi, mila, siasa uchumi, na kadhalika; kwa kawaida lugha huhusiana na mazingira ambamo watu hao wanaishi. Mwingiliano wa jamii kwa kawaida hupelekea jamii moja kukopa dhana zingine ili kufidia upungufu ambao hudhihirika katika utamaduni wao. Lugha kwa kawaida husaidia kuudhibiti uhusiano wa kijamii, lugha ndiyo inayowezesha watu kuwa na maingiliano yenye manufaa. Aidha, kuwepo kwa lugha kunamaanisha kuwepo kwa mtu anayekubalika na jamii yake. Jamii hujengwa na watu tofauti, na lugha ndiyo iwaletayo pamoja na kujenga uhusiano wa kibinafsi katika kiwango cha mtu na mtu, mtu na jamaa yake, na mtu na jamii yake katika shughuli zozote za kitamaduni.

Vijana kama sehemu ya jamii hutumia lugha yao kwa kuegemea maadili ya kijamii na hivyo basi mikakati ya upole katika matumizi yao ya lugha ina ukuruba mpana na maswala ambayo huenda yakachukuliwa kuwa huyafanya matumizi ya lugha ya vijana kusawiri kikundi ambacho hakijali. Kwa mfano, maswala yanayohusiana na sehemu za siri na kazi zake huwakirihisha vijana pia.

## 2.8 VICHOCHEO VYA UCHAGUZI WA MIKAKATI

Paul Grice anadai kwamba wazungumzaji wote ni binadamu razini ambao kimsingi wana haja ya kuuwasilisha ujumbe kikamilifu. Kwa mantiki hii, Brown na Levinson wametumia hoja hii katika Nadharia yao ya Upole kwa kusema kuwa mawakala razini watachagua

mikakati sawia ya upole kama vile wengine katika hali hiyo watajaribu kuunusuru "uso", wameonyesha uwepo wa hali pana katika uneni wenye mikakati ya kurekebisha kupotea kwa uso. Matendo ya kutishia uso *(FTAs)* yana uwezo wa kuafikia kutishia uso, kwa hivyo mawakala razini hujibidiisha kuyazuia matendo ya kutishia uso ama kujaribu kutumia mikakati fulani ya kupunguza tishio.

Mzungumzaji atapima:

1. Haja ya kuwasilisha maswala yaliyomo ya Tendo La Kutishia Uso.
2. Haja ya kuwa stadi au umuhimu wa mambo ya kuwasilishwa.
3. Haja ya kuuhifadhi uso wa msikilizaji kwa kiwango chochote.

Katika hali nyingi za kudhihirisha ushirikiano pale 3 inazidi 2, mzungumzaji atataka kupunguza Tendo La Kutishia Uso.

Hali kubwa ya kuwepo na uwezekano wa kuupoteza uso huhitaji tendo kubwa la kuuokoa. Ikiwa uwezekano wa kuupoteza uso uko katika hali kubwa sana, mzungumzaji huenda akaamua kutupilia mbali Tendo La Kutishia Uso na kutosema lolote.

Kila mkakati huendana na kiwango fulani cha Tendo la Kutishia Uso. Hali fulani inapotokea kuwa hatari zaidi katika kutishia uso, mzungumzaji atatumia mkakati wa kiwango cha juu zaidi ili kuudumisha uso wa msikilizaji wake.

## 2.9 HITIMISHO

Sura hii imezungumzia maswala muhimu ya kimsingi yanayoendana na matumizi ya lugha. Kwanza swala la lugha ya kitamathali limezungumziwa na ambapo ukweli ni kuwa mtumiaji wa lugha huenda akachagua kutumia lugha ya kitamathali katika mazungumzo yake. Swala la lugha na uhusishaji limeangaziwa kwani linahusiana na vile mtumiaji wa lugha huitumia lugha kwa kuihusisha na hali fulani. Uhusishaji huu huendana na kanuni za ubora, idadi, maelezo na mtindo. Katika uhusishaji huu, tumetolea maelezo yake Grice ya kanuni za busara.

Kuchanganya na kuhamisha ndimi ni maswala mengine ambayo yamezungumziwa na kubainisha tofauti iliyoko kati ya dhana zenyewe, katika kuliangazia swala hili tumeliangazia swala la tasifida kama msimbo kwani hali husika huendana na uchanganyaji na uhamishaji wa ndimi.

Uchaguzi wa kileksika kama mojawapo wa kipengele muhimu katika matumizi ya lugha umeangaziwa ambapo swala hili hufumbata pia na utaratibu wake. Lugha pale ambapo mazungumzo ya mzunguko hudhihirika ni sehemu nyingine muhimu ambayo imeangaziwa.

Mazungumzo ya mzunguko hutekelezwa kwa ajili ya ujumbe unaowasilishwa. Majukumu ya kuitumia lugha ya mzunguko hutokana na kukiukwa kwa kanuni za Grice, haja ya mzungumzaji kutaka kudhihirisha ubabe na umoja, matumizi ya mzaha ili kumhusisha

msikilizaji. Swala la lugha na utamaduni limeangaziwa kwani maswala haya ni reale kwa ya pili, mtu anapoitumia lugha huuegemea utamaduni.

Kulikuwa kuna haja ya kuuzungumzia uchaguzi wa mkakati kwani mzungumzaji anapoitumia lugha kuna haja ya kujua kama kuna Tendo La Kutishia Uso, haja ya kuwa stadi na hatimaye haja ya kuuhifadhi uso wa msikilizaji.

# SURA YA TATU

# MIKAKATI YA UPOLE KATIKA MATUMIZI YA LUGHA YA VIJANA.

## 3.1 Utangulizi

Upole ni mfumo wa uhusiano baina ya watu ambao hunuiwa kufanikisha mwingiliano na kupunguza uwezekano wa kutokuelewana na migongano inayoweza kuibuka baina ya binadamu (Brown na Levinson 1987:39). Kwa kifupi, umuhimu wa upole katika mawasiliano ni kudumisha ulinganifu wa kijamii na uhusiano wa kirafiki unaotuwezesha kuchukulia kuwa washiriki katika maongezi wanashirikiana katika ubadilishanaji wa mawazo.

Kuna ukweli kuwa wazo la upole hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine na kutoka sehemu moja hadi nyingine. Vijana huenda vile vile wakawa na njia tofauti za kudhihirisha upole, kwa hivyo jambo huenda likawa ni dhihirisho la upole katika mtazamo mmoja lakini likawa si pole katika mtazamo wa pili.

Sura hii iliangazia baadhi ya mikakati ambayo vijana waliitumia ili kudumisha upole katika maswala ambayo hudhihirika katika mtagusano wa jamii. Pamoja na njia ambazo vijana walitumia ni kama vile; kuhamisha / kuchanganya ndimi, matumizi ya lugha ya siri, kutumia lugha ya mzunguko, lugha ya kitamathali, lugha ya maongezi na uhusishaji, uchaguzi wa msamiati n. k. Majedwali yanayotambulisha mikakati mseto ya upole ya matumizi ya lugha katika matumizi ya lugha kati yao na washiriki wengine katika jamii ilitambulishwa.

### 3.2. Mielekeo ya vijana kuzihusu methali

Wanafunzi tuliotafiti ni wa jinsia zote mbili na lengo la kuwa na methali katika utafiti wetu lilikuwa kuibua uwezekano wa vijana kuelezea hisia zao kuhusiana na vile walivyozichukulia methali zenyewe. Tulitaka kujua kama watafitiwa wangeweza kutambua uwepo wa lugha yenye tasifida au la na maoni yao kuhusiana na methali zenyewe.

Methali husika zilikuwa katika jozi;

*a) Kufa kwa <u>mkundu</u> <u>mavi</u> hutawanyika*

*b) Kufa kwa mdomo mate hutawanyika*

*a) Ukimwiga tembo <u>kunya</u> utapasuka msamba*

*b) Ukimwiga tembo <u>kunya</u> utapasuka <u>mkundu</u>*

Lililodhihirika ni kuwa, vijana walitambua kuwa kati ya methali nne, tatu hazikusawiri picha ya kuwepo na adabu kwani baadhi ya msamiati ulikosa tasifida. Watafitiwa waliyaangazia maneno yaliyopigwa mstari kama yale yaliyodhihirisha lugha chafu. Lugha na utamaduni huwa vipengele muhimu kwa mtumiaji yeyote wa lugha katika jamii.

Kwa mfano; watafitiwa walisema,

*Ni ya aibu kusema,*

*Ina mafunzo lakini inaudhi,*

*Msamiati wake si wa kutajwa ovyoovyo,*

*Haina lugha ya heshima,*

*Ina maneno machafu*

*n.k.*

Kulikuwa na kundi lingine lililosema kuwa methali hizo hazikueleweka.

### 3.3 Mikakati ya lugha kati ya vijana na wazazi wao

Vijana na wazazi wao huchukua nafasi kubwa sana katika maingiliano yao ambapo matumizi ya lugha hudhihirisha mseto wa mikakati ya upole katika matumizi yao ya lugha, ukweli huu una mashiko. Maswala tuliyoangazia huibuka katika jamii, na kwa hivyo hiki ni kigezo mwafaka cha kubainisha ukweli kuwa vijana hutumia mikakati ya upole katika matumizi yao ya lugha. Kuwepo kwa mseto wa mikakati kunatokana na ukweli kuwa mada zinatofautiana, washiriki, tukio n.k, swala la jinsia vile vile lilichangia kwa kiwango kikubwa.

Majedwali haya mawili yanatoa picha ya vile wavulana na wasichana walivyokabiliana na udadisi uliowahusu wazazi wao. Majedwali yenyewe yanabainisha kuwa mikakati ilikuwa inatofautiana na kudhibitisha kuwa vijana huitumia mikakati tofauti wanapowasiliana na wazazi wao.

*UFUNGUO*

| | |
|---|---|
| A-Methali | K-Swala la wizi |
| B-Uvutaji wa sigara | L-Swala la kujamiiana |
| C-Swala la hedhi | M-Swala la kushuta |
| D-Swala la maliwato | N-Swala la simu ya mchumba |
| E-Swala la fedha | O-Swala la mkao mbaya |
| F-Swala la kuchumbiana | P-Swala la njia na dharura |
| G-Mgonjwa wa UKIMWI | Q-Swala la ubakaji |
| H- Swala la mapenzi yenye ila | R-Swala la kunya pasipofaa |
| I-Swala la zipu | S-Swala la jina la sehemu za siri |
| J-Swala la tanzia | T-Swala la kutusi |

Wtf-(wavulana 15, wasichana, 15) = watafitiwa 30

Jedwali la 1

Wavulana na wazazi wao

| wtf | A | B | C | D | E | J | M | N | O | P | R | S | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 1 | 3 | 1 | 4 | 1 |
| 2 | 5 | 1 | 4 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | * | 4 | 4 |
| 3 | 6 | 1 | 1 | 1 | 3 | 4 | 3 | 3 | 4 | 3 | 1 | 1 | 4 |
| 4 | 5 | 1 | * | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 2 | * | 4 | 1 |
| 5 | 5 | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | 4 | 4 | 1 |
| 6 | 6 | 1 | * | 4 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | 1 | 4 | 4 |
| 7 | 5 | 3 | * | 3 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | * | * | 4 |
| 8 | 5 | 4 | 1 | 4 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | 1 | 4 | 4 |
| 9 | 5 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 1 | 3 | 1 | 4 | 4 |
| 10 | 6 | 3 | * | 3 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 4 |
| 11 | 5 | 3 | 4 | 4 | 3 | 4 | 3 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 |
| 12 | 6 | 1 | 4 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 4 |
| 13 | 6 | 1 | 4 | 4 | 1 | 4 | 4 | 3 | 1 | 3 | 1 | 4 | 1 |
| 14 | 6 | 1 | 1 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 |
| 15 | 5 | 3 | 4 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 3 | 4 | 4 | 4 |

<u>UFUNGUO</u>

1 - Kuwa kwenye rekodi (mkakati unaoyasema mambo kama yalivyo).

2 -Upole chanya (mkakati unaozuia mgongano, uwepo wa urafiki,umoja).

3 -Upole hasi (njia za kudhihirisha uhuru kwa msikilizaji).

4 -Kuwa nje ya rekodi (mkakati usiokuwa wa moja kwa moja).

5 -Hazijatumia lugha safi, yenye adabu na kadhalika.

6 - Hazieleweki.

*Kutofanya Tendo La Kutishia Uso

Jedwali la 2

Wasichana na wazazi wao

| wtf | A | B | C | D | E | J | M | N | O | P | R | S | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5 | 1 | 1 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 3 | 4 | 4 |
| 2 | 6 | 1 | 3 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 3 | 4 | 4 |
| 3 | 5 | 3 | 3 | 3 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 3 | 4 | 4 | 4 |
| 4 | 6 | 1 | 3 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 1 |
| 5 | 5 | 1 | 4 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | 4 | 4 | 4 |
| 6 | 5 | 3 | 1 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 |
| 7 | 5 | 1 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 | 3 | 4 | 1 | 3 | 4 | 4 |
| 8 | 5 | 1 | 3 | 1 | 2 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 4 |
| 9 | 5 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 4 | 3 | 4 | 4 | 4 |
| 10 | 5 | 1 | 3 | 1 | 3 | 4 | 4 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 |
| 11 | 5 | 1 | 3 | 4 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 1 | 4 | 4 | 4 |
| 12 | 6 | 3 | 3 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 4 | 3 | * | 4 | 4 |
| 13 | 6 | 3 | 3 | 1 | 3 | 4 | 3 | 3 | 4 | 1 | * | 4 | 1 |
| 14 | 6 | 3 | 3 | 1 | 3 | 1 | 4 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 4 |
| 15 | 5 | 1 | 4 | 1 | 3 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 4 |

## 3.4 Mikakati ya lugha kati ya vijana na walimu

Vijana na walimu ni sehemu nyingine muhimu katika jamii ambapo matumizi ya lugha hudhihirika sana. Majedwali haya yametambulisha kwa yakini uwepo wa mseto wa mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana wanapowasiliana na walimu wao. Mada na jinsia ni kipengele muhimu ambacho kilipelekea kuelekeza ni mkakati upi ambao ulitumiwa na vijana wanapoelezea namna ya kuwasiliana na walimu. Tofauti baina ya wavulana na wasichana ni bayana kama inavyosawiriwa kwenye majedwali. Ni dhahiri kuwa mikakati ya kuwa nje ya rekodi na upole hasi ilipendelewa sana na vijana dhidi ya walimu wao.

Jedwali la 3

Wavulana na walimu wao

| wtf | B | D | G | H | I | J | K | L | M | P | S |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 4 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 3 | 3 | 3 | 4 |
| 2 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 3 | 1 | 3 | 1 | 4 | 3 | 1 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 |
| 4 | 1 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 5 | * | 3 | 3 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 6 | 1 | 1 | 3 | 4 | 4 | 1 | 4 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 7 | 1 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | * |
| 8 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 9 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 4 |
| 10 | 3 | 3 | 1 | * | 1 | 3 | 1 | * | 3 | 3 | 4 |
| 11 | 1 | 3 | 4 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 12 | 4 | 1 | 2 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 13 | 1 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 14 | 4 | 1 | 3 | 3 | 4 | 1 | 1 | 4 | 3 | 1 | 4 |
| 15 | 1 | 3 | 2 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 4 | 3 | 4 |

Jedwali la 4

Wasichana na walimu wao

| wtf | B | D | G | H | I | J | K | L | M | P | S |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 2 | 4 | 3 | 4 | 4 | 3 | 4 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 3 | 3 | 3 | 3 | 4 | 3 | 4 | 3 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 4 | 3 | 3 | 4 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 5 | 4 | 3 | 2 | 4 | 3 | 1 | 4 | 4 | 4 | 3 | 4 |
| 6 | 3 | 3 | 4 | 4 | 3 | 3 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 7 | 4 | 3 | 2 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 8 | 3 | 3 | 4 | 4 | 3 | 4 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 9 | 3 | 3 | * | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 3 | 1 | 4 |
| 10 | 2 | 3 | 4 | 4 | 1 | 4 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 11 | 4 | 3 | 4 | 4 | 1 | 4 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 12 | 3 | 3 | 4 | 4 | 3 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 13 | 2 | 4 | 4 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 14 | 4 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| 15 | 3 | 4 | 4 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 |

### 3.5 Mikakati ya lugha kati ya vijana na marafiki zao

Urafiki na matumizi ya lugha baina ya marafiki ni sehemu nyingine ambayo ilidhihirisha uwepo wa matumizi tofauti tofauti ya mikakati ya upole baina ya vijana. Vijana wa kiume na kike wanayo mikakati ambayo ilitofautiana kulingana na mada. Picha inayosawiriwa na majedwali ni kuwa vijana waliipendelea mikakati ya kuwa kwenye rekodi, upole hasi na kuwa nje ya rekodi.

Jedwali la 5

Wavulana na marafiki zao

| wtf | B | C | D | E | F | G | H | I | J | K | L | M | P | Q | R | S | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 4 | 4 | 3 | 3 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 2 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 3 | 1 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 4 | 1 | 1 | 2 | 2 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 4 | 1 | 2 | 1 | 3 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 4 | 1 | 4 | 4 |
| 5 | 1 | 2 | 1 | 3 | 3 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 3 | 4 | 1 | 4 | 1 |
| 6 | 1 | 4 | 4 | 3 | 3 | 3 | 4 | 1 | 4 | 4 | 4 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 7 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 |
| 8 | 1 | 4 | 4 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 9 | 1 | 4 | 4 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 10 | 1 | * | 1 | 1 | 3 | 1 | 4 | 1 | 4 | 1 | * | 4 | 3 | 1 | 4 | 4 | 4 |
| 11 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 12 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 2 | 4 | 1 | 1 | 1 | * | 4 | 1 | 4 | 1 | 4 | 1 |
| 13 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 14 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 2 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 |
| 15 | 4 | 4 | 1 | 3 | 3 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 1 |

Jedwali la 6

Wasichana na marafiki zao

| wtf | B | C | D | E | F | G | H | I | J | K | L | M | P | Q | R | S | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 3 | 3 | 4 | 4 | 4 | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 2 | 4 | 1 | 4 | 1 |
| 3 | 3 | 3 | 1 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 4 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 2 | 3 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 5 | 4 | 3 | 1 | 1 | 3 | 2 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 6 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 7 | 1 | 4 | 1 | 2 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 8 | 1 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 4 | 1 |
| 9 | 1 | 4 | 1 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 | 2 | * | 1 | 3 | 1 | 1 | 3 | 4 | 1 |
| 10 | 1 | 4 | 1 | 1 | 3 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 11 | 1 | 4 | 1 | 2 | 3 | 1 | 4 | 4 | 4 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 12 | 1 | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 13 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 14 | 1 | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 1 |
| 15 | 1 | 4 | 1 | 3 | 3 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 | 1 | 4 | 4 | 1 |

## 3.6 Mikakati ya lugha kati ya vijana na watu wasiowajua

Matumizi ya lugha kati ya washiriki wawili ambao hawajuani iliweza kuibua mielekeo tofauti ambayo iliegemea mada. Jambo la kimsingi lililoibuka ni kuwa mikakati husika katika mawasiliano ni ya mseto na vile vile msemaji alitokea kunyenyekea au hata akakosa makini kutokana na kile alichozungumzia kwani ikiwa ameudhiwa uchaguzi wake ulikuwa tofauti na pale alitaka usaidizi.

Jedwali la 7

Wavulana na watu wasiowajua

| wtf | B | C | E | J | P | R | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 1 |
| 2 | 1 | 1 | 3 | 4 | 3 | 1 | 1 |
| 3 | 1 | 1 | 3 | 3 | 3 | 1 | 1 |
| 4 | 1 | * | 3 | 1 | 3 | 1 | 1 |
| 5 | * | 2 | 3 | 1 | 3 | 1 | 1 |
| 6 | 1 | * | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| 7 | 3 | * | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 |
| 8 | 4 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| 9 | 3 | 4 | 3 | 4 | 3 | 4 | 4 |
| 10 | 3 | * | 3 | 4 | 3 | 3 | 4 |
| 11 | 1 | 4 | 3 | 4 | 3 | 1 | 1 |
| 12 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 1 | 4 |
| 13 | 1 | 4 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 |
| 14 | 1 | 4 | 3 | 4 | 1 | 4 | 1 |
| 15 | 4 | 4 | 3 | 1 | 3 | 4 | 1 |

Jedwali la 8

Wasichana na watu wasiowajua

| wtf | B | C | E | J | P | R | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 4 |
| 2 | 3 | 3 | 3 | 3 | 4 | 1 | 4 |
| 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 |
| 4 | 4 | 3 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 |
| 5 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 1 |
| 6 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 4 |
| 7 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 |
| 8 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 |
| 9 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | * | 4 |
| 10 | 1 | 4 | 3 | 4 | 3 | 1 | 1 |
| 11 | 1 | 4 | 3 | 3 | 3 | 3 | 1 |
| 12 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 |
| 13 | 3 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 |
| 14 | 2 | 4 | 3 | 3 | 3 | 2 | 1 |
| 15 | 4 | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 1 |

## 3.7 Mikakati ya lugha kati ya vijana na watoto, daktari na mgonjwa wa Ukimwi

Mada na washiriki katika mawasiliano ziliibua mseto wa mikakati ya upole ya lugha waliyoitumia vijana, tendo hili lilitokea kuisawiri picha tofauti kwani utumiaji wa mkakati mmoja uliegemea tofauti ya kiumri na tukio lililokuwa likiangaziwa. Swala la jinsia lilielekeza hali ya vile maswala yalishughulikiwa.

Jedwali la 9

Wavulana na watoto wadogo kushuta, kunya, kutusi, sehemu za siri / mgonjwa wa ukimwi / mgeni na sigara/ daktari na sehemu za siri**

| wtf | B | | G | | M | | S | | R | S | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3 | | 3 | | 3 | | 1** | | 1 | 4 | 1 |
| 2 | 1 | | 2 | | 3 | | 1** | | 1 | 4 | 1 |
| 3 | 3 | | 2 | | 4 | | 1** | | 4 | 4 | 1 |
| 4 | 3 | | 3 | | 3 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 5 | 1 | | 3 | | * | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 6 | 4 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 7 | 3 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 8 | 4 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 9 | 1 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 10 | 3 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 11 | 1 | | 3 | | 4 | | 4** | | 4 | 4 | 1 |
| 12 | 3 | | 2 | | 3 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 13 | 3 | | 2 | | 3 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 14 | 3 | | 3 | | 4 | | 4** | | 4 | 4 | 1 |
| 15 | 4 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |

Jedwali la 10

Wasichana na watoto wadogo kushuta, kunya, kutusi sehemu za siri / mgonjwa wa ukimwi / mgeni na sigara/ daktari na sehemu za siri**

| wtf | B | | G | | M | | S | | R | S | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3 | | 3 | | * | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 2 | 2 | | 3 | | 1 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 3 | 3 | | 3 | | 3 | | 4** | | 1 | 1 | 1 |
| 4 | 3 | | 3 | | 1 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 5 | 1 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 6 | 3 | | 3 | | 3 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 7 | 3 | | 3 | | 1 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 8 | 3 | | 1 | | 4 | | 4** | | 1 | * | 1 |
| 9 | 3 | | 3 | | 4 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 10 | 3 | | 2 | | 3 | | 4** | | 2 | 4 | 1 |
| 11 | 3 | | 2 | | 4 | | 4** | | 1 | * | 1 |
| 12 | 3 | | 3 | | 2 | | 4** | | 1 | 4 | 1 |
| 13 | 1 | | 3 | | 4 | | 4* | | 1 | 4 | 1 |
| 14 | 1 | | 3 | | 3 | | 4* | | 1 | 4 | 1 |
| 15 | 3 | | 3 | | 4 | | 4* | | 1 | 4 | 1 |

## 3.8 Mikakati ibuka katika matumizi ya lugha ya vijana katika utafiti

Tukio moja ambalo limedhihirika bayana katika utafiti huu ni kuwa vijana wanatambua uwepo wa lugha iliyo na adabu. Vijana vile vile wamedhihirisha umilisi wao katika kuitumia mikakati tofauti ya upole wanapowasiliana na makundi tofauti tofauti katika jamii. Ili

kulidhihirisha tukio hili bayana tunaangazia mseto wa mikakati ya upole iliyoibuka katik matumizi ya lugha ya vijana.

### 3.8.1 kuchanganya / Kuhamisha ndimi

Kuchanganya na kuhamisha ndimi ni maswala ya kimsingi tuliyoyaangazia waziwazi na jin yanavyotokea. Wamitila (2003b: 195) ameziangazia dhana hizi kwa kusema, kuchangany ndimi ni mbinu ambapo mwandishi anatumia lugha mbili au zaidi kwa kuchangany Sababu kuu ni kuonyesha tofauti za wahusika kwa matumizi ya lugha. Huweza kutumiv kama kinaya pale ambapo mhusika anayechanganya ndimi anaitumia lugha fulani vibay Anasema kuwa tofauti kati ya kuhamisha ndimi na mbinu iliyotangulia ni kuwa hap msemaji anaacha lugha fulani na 'kuhamia' kwenye lugha nyingine. Mhusika anaitum lugha fulani bila ya kuingiza maneno ya lugha ya pili ndani. Sababu za kuitumia mbinu zinafanana na za kuchanganya ndimi.

### 3.8.2 Vijana na ubadilishaji / uchanganyaji wa ndimi

Vijana kama sehemu ya jamii walitokea kudhihirisha wingi wa uchanganyaji wa lugha kati matumizi yao ya lugha. Katika utafiti wetu tulikumbana na maneno kama vile; Kuhusiana hedhi kuna matumizi kama haya ya lugha;

| Kuwa kwenye rekodi | Upole chanya | Upole hasi | Kuwa nje ya rekodi | Kuzuia tendo la kutishia uso |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| *M.p* iko *ready*<br><br>*Skirt* ina *m.p,* | | Nguo ime*soil,*<br><br>Nguo ime*soak,*<br><br>Vipi *madays,*<br><br>Ni aje *periods,*<br><br>Tafuta *always* | *Valentine* ili*drop,*<br><br>*Red carpet,*<br><br>*Punch,*<br><br>Una *visitor,*<br><br>umeji*rainia* | |

Swala la hedhi katika jamii huwa ni mwiko na kwa kawaida halitajwi ovyoovyo. Kutokana na ukweli huu vijana walitokea kubadilisha na kuchanganya ndimi ili kudhihirisha upole. Wale ambao wametokea kuitaja hali hiyo kwa kutumia neno 'damu' bila shaka watachukuliwa kuwa watovu wa adabu. Kuchanganya na kubadilisha ndimi ni mojawapo wa mkakati wa vijana wa upole katika matumizi ya lugha.

Katika matumizi yao ya lugha vijana walilichukulia swala la ukimwi kwa njia ambayo ilidhihirisha kuwepo kwa mkakati wa upole kwani kuchanganya na kuhamisha ndimi kuliyapunguza makali katika lugha.

| Kuwa kwenye rekodi | Upole chanya | Upole hasi | Kuwa nje ya rekodi | Kuzuia tendo la kutishia uso |
|---|---|---|---|---|
| Pole *he is HIV*, | | Atumie *ARVS*,<br>*Imagine* utapona | *Atleast* anaweza,<br>*Health* yake ni *poor*,<br>Mnasa*il* kwa *same boat*, | |

Swala la UKIMWI huogofya na mtu anapowasiliana na mwingine hulazimika kudhihirisha upole kwa walioathiriwa na hali hiyo. Vijana walitokea kuchanganya ndimi ili kusawiri dhana ya upole katika matumizi yao ya lugha.

### 3.8.3 Vijana na matumizi ya misimbo

Kujadili mambo ya siri kunaweza kuafikiwa kwa kuelewa tasifida zinazoeleweka na wachache. Wazazi wakati mwingine huisafidi lugha wanapozungumzia maswala ya watu wazima hata kama wana wao wako karibu. Vijana nao hubuni maneno misimbo na msamiati ili kuwasiliana kisiri hata kama kuna watu wengine. Buliba na wenzake (2006:73) wanasema kuwa ubadilishaji msimbo si jambo la hiari, bali ni mbinu inayotumika kulingana na mada na hali iliyopo.

Utafiti wetu umebainisha kuwa vijana hutumia misimbo fulanifulani ili kutajia mambo ambayo hukirihisha pale yanapotokea kutajwa moja kwa moja. Swala kuhusiana na jina

jingine ambalo wanaweza kutajia sehemu za siri liliibua ukweli kuwa kunayo majina badalia ya kimsimbo ili kufidia makali katika matumizi yao ya lugha;

| Msimbo | kusimamia |
|---|---|
| Kuro | Malaya |
| Sekta | Uke |
| Njwanga | Uume |
| Pakususu | Uke/ uume |
| Madude | Uume |
| Patakatifu | Uke |
| 'Cargo' | Uume / uke |
| Makei | Hasua / korodani |
| Mgondi | Mwizi |
| Doo | Pesa |
| Monde | Pesa |
| Luu | Choo |
| Dedi | Kufa |

### 3.8.4 Tasifida kama mkakati wa upole

Kujadili mambo ya siri kunaweza kuafikiwa kwa kuelewa tasifida zinazoeleweka na wachache. Vijana wakati mwingine huisafidi lugha wanapozungumzia maswala yanayoweza kuibua hisia kuwa vijana hawana adabu katika matumizi yao ya lugha. Ili kudhihirisha upole vijana hubuni maneno misimbo na msamiati ili kuwasiliana kisiri hata kama kuna watu wengine. Katika utafiti wetu tuliweza kujua kuwa matumizi ya maneno yenye tasifida kulibainika, bila shaka huu ni mkakati wa upole ambao unawasawiri vijana kama kikundi

ambacho kinatambua umuhimu wa kuitumia lugha yenye chembechembe za upole. Kwa mfano,

'Msalani' badala ya choo,

'Amepumzika' badala ya kufa,

'Kunanyesha' badala ya unatokwa na damu (hedhi)

'Cheki manguo yako' badala ya kaa vizuri,

'Amegenya' badala ya amekufa,

Lililo muhimu ni kuwa vijana wamedhihirisha kuwa kuna lugha ya upole na isiyokuwa ya upole, hivyo basi kudhihirisha kuwa wanayo mikakati ya kuangazia maswala ambayo yanaweza kuwasawiri kama watovu wa adabu.

### 3.8.5 LUGHA YA MZUNGUKO

Kuzungumza kwa njia ya mzunguko kuna majukumu mengi katika mawasiliano; hujaribu kupunguza migongano, kuingiza hila katika habari, kuingiza mzaha katika maongezi, kutoeleza mambo kwa ukamilifu wake, (yaani kutosema ukweli). Kwa kawaida msikilizaji huchukuliwa kuwa atamwelewa mzungumzaji hata kama haelezewi mambo moja kwa moja.

Lakoff (1973, 1979) anasema kuwa maelezo ya mzunguko kwa kawaida yanashtahiwa kwa ajili ya sababu mbili kuu; kuuokoa uso kama mchango ili kuipa hisia ya maelewano inayopatikana kwa kueleweka bila kusema kile mzungumzaji anachokimaanisha. Zaidi ya hayo, mzungumzaji anapodhamiria msikilizaji au msomaji ajijazie maana fulani katika

maelezo fulani, njia ya mzunguko hupelekea kumshirikisha msikilizaji au msomaji, hivyo kuwepo kwa maelewano ya pande mbili.

Vijana katika mazungumzo yao huitumia lugha ya mzunguko ili kuudhihirisha upole kati yao na watu wengine. Lugha ya vijana ya mzunguko haitumiwi kila mahali na haihusishi kila mtu, la hasha! Mambo kadha wa kadha huchangia; vile vile sehemu kubwa huelekeza namna lugha ya mzunguko itakavyotekelezwa, swala la umri, jinsia na mada ni muhimu mno katika kuelekeza vile lugha inavyotumiwa.

Mkakati wa Brown na Levinson (1987) wa Kuwa Nje ya Rekodi ni kipengele muhimu katika kuitathmini mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana katika utafiti wetu, kwani lugha ya mzunguko iliisheheni kazi yetu popote pale maswala yenye kukirihisha jamii yaliangaziwa. Utafiti umebainisha namna vijana huitumia lugha ya mzunguko ili kuwasiliana kwa njia ya upole.

Utafiti ulikusudia kupata jina ambalo vijana wanaweza kuzitajia sehemu za siri, lililotokea kudhihirika ni kuwa watafitiwa walitumia lugha ya mzunguko ili kuwasiliana kwa njia ya upole;

| Kuwa kwenye rekodi | Upole chanya | Upole hasi | Kuwa nje ya rekodi | Kuzuia tendo la kutishia uso |
|---|---|---|---|---|
| | | ➢ Naumwa nikienda kukojoa.<br>➢ Nimeumia katikati ya miguu. | ➢ Jamani nimeumia huku *down.*<br>➢ Nimeumia *down* chini.<br>➢ Nimeumia mahali pabaya.<br>➢ Nimeumia mahali hapasemeki kwa umati<br>➢ Nimeumia *place* zingine *painful.*<br>➢ *My 'ninino' is paining.*<br>➢ Naumia huko.<br>➢ Hizo *parts* hazi*feel* poa.<br>➢ Nimeumia sehemu nyeti | |

Crystal (2000:63) alizungumzia *'lugha ya kuambaa'* ambapo alisema matamshi huenda yakabadilika kutokana na mwingiliano wa miiko lugha... kwa sababu lugha ni mali ya jamii ni vizuri kusema kuwa jamii ndiyo ambayo huamua neno la kusemwa ni lipi na lisemwe wapi. Buliba na wenzake (2006:90) wamesema kuwa ... huamuliwa na utamaduni neno huwa linakufuru ikiwa linasababisha hisia mbaya kwa msikilizaji au linataja maneno ya siri, n.k.

Vijana waliyatumia maneno ya mzunguko kama njia ya kuitajia sehemu ya siri na kukosa kutoa jina moja lililotarajiwa, huku ni kuzunguka ambako kulidhihirisha matumizi ya lugha ya upole. Swala la hedhi vile vile lilitokea kithibitisha kuwa vijana hutumia lugha ya mzunguko pale umri unatokea kuwazidi, vile vile katika mazungumzo kati yao na wazazi wao. Lugha ya

mzunguko na kuambaa ni maneno mamoja ambayo yana sehemu yake katika jamii, vijana ni sehemu ya jamii; kwa mfano,

| Kuwa kwenye rekodi | Upole chanya | Upole hasi | Kuwa nje ya rekodi | Kuzuia tendo la kutishia uso |
|---|---|---|---|---|
| | | ➢ Mama una uchafu nyuma.<br>➢ Nadhani nguo yako imechafuka nyuma.<br>➢ Mama una unyevunyevu.<br>➢ Mam ni nini *skirt* yako imefanya? | ➢ Mama *there is someone at your back.*<br>➢ Si uende ujisaidie.<br>➢ Mama umekalia nini?<br>➢ *Excuse*, angalia nguo yako nyuma.<br>➢ Si uende hospitali utibiwe.<br>➢ Tafuta *always* | |

### 3.8.6 Maongezi na uhusishaji

Dhana ya kimsingi katika maongezi ni; labda kama imedokezwa vinginevyo, ni kuwa washiriki lazima wazingatie kanuni za kushirikiana na mikakati (Yule1996:40). Ni jambo muhimu kujua kwamba ni mzungumzaji ambaye huwasiliana kupitia uhusishaji, na ni msikilizaji anayeng'amua maana kutokana na yale yaliyowasilishwa. Uchaguzi wa yaliyosemwa huegemea yale ambayo yana uwezo wa kudumisha malengo ya kushirikiana.

Kanuni za kushirikiana za Grice (1975) hudokeza namna mtu huweza kuusimbua ujumbe kulingana na wengine wanavyosema. Ili mtu aweze kuisimbua habari ya mzungumzaji vizuri huegemea mtazamo wake Grice ambao aliuita kanuni za majadiliano na ambao uliangaziwa upya na Levinson (1983) ambapo hatua tano hubainika:

- Kanuni ya ushirikiano.
- Kanuni ya ukweli.
- Kanuni ya idadi.
- Kanuni ya uhusiano.
- Kanuni ya mtindo

Kwa kifupi, kanuni hizi hudokeza namna washiriki katika mazungumzo wanaweza kujadiliana kwa kuegemea kanuni kisawasawa, kirazini na kwa njia ya kushirikiana; wazungumze kwa kuegemea ukweli, kwa kuegemea uhusiano wa kile kinachosemwa na kwa njia ya wazi ili kuitoa habari toshelevu (Levinson k.h.j:102- 3). Katika mazungumzo yao na kutokana na matokeo yetu ni wazi kusema kuwa vijana waliongozwa na kanuni hizi bila ya wao kutambua; kwa hakika hii tutaichukulia kuwa silika ya kibinadamu.

Mikakati ya upole ya vijana wanayotumia kwa kiwango kikubwa ilitokea kuzingatia kanuni za kushirikiana; Ikitokea hili halifanyiki basi kanuni hizi huenda zikawa zimekiukwa hivyo basi yaliyokuwa yakitarajiwa katika mawasiliano yakatokea kutoafikiwa. Hofmann (1993:287) anasema kuwa kukiukwa kwa kanuni za maongezi hudhihirisha kuwa wazungumzaji wanalifanya jambo lingine na sio tu kutoa ripoti kuhusu ukweli: wanayosema huenda yakaangaziwa kupitia ufasili mzuri wa sheria. Kimsingi maswala kama haya yataashiria

kuzingatiwa kwa kanuni za ushirikiano ikiwa ujumbe unaolengewa msikilizaji utafasilika. Kwa mfano, kunao ushirikiano baina ya wazazi na vijana;

Mam ni nini *skirt* yako imefanya.

*Imagine* Carol alikufa.

Aki mam umeniboo.

Nimeumia sehemu nyeti.

Sasa mam ninataka ku*buy* kitu siuni*help* doo.

Nataka pesa.

Kwa kuangazia matukio kama haya kunao ukweli kuwa, upo ushirikiano baina ya namna vijana na wazazi wao huwasiliana.

Kanuni ya ukweli ilitokea kudhihirika kwa kiwango fulani kwani maswala ambayo yalikuwa nyeti yaliwapelekea vijana kuitumia lugha ya mzunguko ili kuuwasilisha ujumbe. ***Kunayo matumizi ya madanganyo ya upole hasa pale wanapotokea kulitoa jibu la kuwa simu waliyopigiwa ilitoka kwa rafiki yao wa shule.*** Mkakati huu kulingana nao Brown na Levinson ni mojawepo wa matumizi ya Upole Hasi kwani msikilizaji ambaye ni mzazi atatokea kuyaafiki maelezo hayo hata kama amedanganywa. Kuyaafiki mawazo haya kutatokea kudhihirisha kuokolewa kwa Uso Hasi wa mzazi.

Kutokana na tukio kama hili ukweli uliopo ni kuwa vijana kwa kawaida hutumia mikakati ya upole kuwahadaa washiriki wao pale kulipo na Tendo La Kuutishia Uso wa msikilizaji.

### 3.8.7 Lugha ya kitamathali kama tasifida katika matumizi ya lugha ya vijana

Kama vile ilikwisha elezewa lugha ya kitamathali haielezi mamabo moja kwa moja lakini huongezea vidato vya kimaana katika matumizi fulani ya lugha. Katika matumizi yao ya lugha vijana walidhihirisha upole kwa kuitumia lugha ya kitamathali kama tasifida. Ikumbukwe kuwa tasifida inayo majukumu mengi: inaweza kutumiwa kama njia moja ya kuudumisha ushirikiano, kuongezea hadhi katika mazungumzo ya kawaida vile vile inaakisi umuhimu wa maadili fulani. Kwa kifupi, tasifida hupunguza msuguano katika mawasiliano na kuleta mlahaka mzuri kwa watumiaji wa lugha.

Katika lugha ya Kiswahili kunazo tasifida chungu nzima zinazoendana na "kifo". Mazoea ya kuzitumia tasifida za kifo zinaingiliana na utamaduni wa jamii kwani jina "kifo" ni mwiko na kulitajataja ni kama kukiashiria kifo.

Katika mikakati ya Upole ya matumizi ya lugha ya vijana kulikuwa na tamathali kama,

Ameaga dunia,
*Kicked the bucket,*
Amekata kamba,
*Passed away,*
Ametuacha mkono,
Amekata roho,
Ameenda jongomeo,
Ameipa dunia kisogo
n. k.

Tamathali zingine zilitokana na matumizi ya lugha pale vijana walitaka kwenda haja ambapo walisema,

Naenda kukata,
Kupunguza uzito
n.k.

Wizi ulielezwa na vijana kwa matumizi ya kitamathali kama,

Mkono mrefu,
Mpiga *tero,*
n.k.

### 3.8.8 Utafutaji wa fadhila

Brown na Levinson wameongezea maelezo kuhusiana na Upole Hasi wanapouita Utafutaji wa Fadhila, au mzungumzaji kuomba msikilizaji fadhila. Huu ni mfano ulio dhahiri wa mikakati hasi ya upole inayotumika. Kuna hatua tatu za utafutaji wa fadhila:

- Hatua ya matayarisho,
- Hatua ya kulenga na
- Hatua ya mwisho.

Kutokana na utafiti wetu, msimamo wa Brown na Levinson ulidhihirika bayana kwani swala la kutanguliza mawasiliano ili kuweka njia ya kutafuta urafiki wa kiuchumba na kijana wa jinsia tofauti lilidhihirisha mbinu hii ya utafutaji wa fadhila.

Kwa mfano;

*You see* nilikuwa nili... kuwa ninataka kukuambia...*okay I don't know how you will take it...*

Niaje? Haki kuna vile umeiva tu kimpango.

Sasa, naweza kuongea na wewe *one minute...please* usinilenge...

Niaje mimi naitwa ... *may be,* ningependa kukujua.

Utafiti wetu ulitambua kuwa vijana wa jinsia zote hutamaniana kiasi cha kuutumia mkakati huu ili kuanzisha harakati za usuhuba. Nakubaliana nao Brown na Levinson kwani maelezo yao yamedhihirika wazi.

Kuwepo kwa Utafutaji wa Fadhila kumeangaziwa na Carter na McCarthy (1994) kwa kutolea mfano ambao unayaafiki matokeo yetu. Kulingana na mtazamo wao pia, Utafutaji huu wa Fadhila unahusiana na mkakati wa Upole Hasi.

### 3.9 Hitimisho

Sehemu hii imeangazia baadhi ya mikakati iliyotumiwa na vijana katika matumizi yao ya lugha. Ukweli ambao ulibainika ni kuwa vijana hutokea kuitumia mikakati mseto katika matumizi ya lugha katika mawasiliano. Tumedhihirisha kuwa mikakati ibuka huegemea maswala kadha wa kadha kama vile, Maongezi na uhusishaji, lugha ya mzunguko, Vijana na matumizi ya misimbo, Vijana na Kuhamisha / kuchanganya ndimi, lugha ya kitamathali kama tasifida, na pia kama msimbo, utafutaji wa fadhila, maelezo yetu yalitanguliwa na maelezo ambayo yalidhamiriwa kutoa mwanga kuhusiana na namna mikakati hii ilivyotokea kutenganisha sehemu mbili muhimu, ile ya wavulana na wasichana.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA MATOKEO YA TOFAUTI YA MATUMIZI YA MIKAKATI YA UPOLE KWA VIJANA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inachanganua matokeo ya tofauti ya matumizi ya mikakati ya upole katika lugha ya vijana. Kutokana na yale ambayo tumeangazia ni kuwa matumizi ya mikakati hii inaashiria kuwa vijana hutumia mikakati ya mseto katika matumizi ya lugha yao. Sura yenyewe itaangalia tofauti hii kwa kuegemea maelezo ya asilimia ili kudhihirisha kuwa tofauti iliyoko katika mikakati ni bayana.

## 4.2 Uwepo wa Uso katika ujana

Dhana ya 'uso' imechukua nafasi mwafaka katika kuielezea Nadharia Ya Upole; Brown na Levinson kwa mfano waliiteua kama kiungo kinachokubalika kote katika utafiti na utumizi wa lugha na tukio la upole (1978, 1987). Wamefafanua 'uso' kama "picha ya mtu - binafsi katika macho ya umma ambapo kila mmoja hupenda kumdhihirisha yeye, lakini kwa kawaida wanamaanisha 'uso' kama "picha ya mtu mbele ya umma" na karibu katika matini yao yote wametumia istilahi ya 'uso' ikilinganishwa na "picha ya mtu mbele ya umma" ambayo imetumiwa kwa kiwango kidogo. Brown na Levinson wamezalisha wazo la "uso' kutoka kwa Ervin Goffman na kutoka kwa istilahi ya jadi ya Kiingereza ambayo inafungamana na mwingiliano wa mawazo ya uso ya kutahayarishwa au kudhalilishwa, au "

kuupoteza uso"(1978). Kutokana na uchanganuzi wao wametofautisha kati ya Uso Hasi na Uso Chanya ambapo ni:

a) Uso Hasi: madai ya kimsingi ya maeneo, kusetiri mambo ya kibinafsi, haki ya kutotofautisha - kama vile uhuru wa kutenda na uhuru wa kutolazimishiwa.

b) Uso Chanya: kuendelea kudumisha picha chanya ya mtu binafsi au 'utu' (muhimu sana inahusisha kuwapo na haja ya picha ya mtu kukubalika) katika mtagusano wa wanaoshiriki (1978:66).

Uso Hasi na Uso Chanya waweza kuelezewa kama Mahitaji, yaani, uso hasi: uhitaji wa kila 'mhusika aliyekomaa na mwenye uwezo' kuwa maamuzi yake hayatakinzwa na wengine, uso chanya: uhitaji wa kila mhusika kuwa mahitaji yake yatapendeza watu wengine kwa kiasi.

'Uso' ni 'sitiari tunayoishi kwayo,' kama wanavyosema Lakoff na Johnson (1980). Inaturuhusu sisi watendaji na watazamaji pamoja, kuelewa mambo muhimu ya matukio ya upole. Inaamsha hisia za hatari katika mtagusano wa asili wa kijamii, uwezekano wa kutishiwa na kuumizwa katika msimamo wa kijamii au uadilifu wa mtu - na zaidi ya hayo, inatukumbusha kuwa uwezekano wa kudhuriwa kijamii ni wa sehemu mbili.

Kama vile Brown na Levinson walivyoashiria kila mtu ana uso na uso wa kila mtu unategemea kusitiriwa kwa uso wa mtu mwingine, na kwa sababu watu hutarajiwa kuusetir

uso wao wakati wametishiwa, na ikiwa kuusitiri wao kutatishia nyuso za wengine, ni jambo la kijumla katika kila mshiriki kusitiri uso wa mwenzake( 1978:66).

Vijana kama sehemu ya jamii ina uso wa kusitiriwa na hisi chanya za kuzisetiri nyuso za wengine bila shaka kutokana na utafiti wetu tumeweza kubainisha kuwa mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana ipo, ni ya mseto lakini kiwango kikubwa kimeegemea Uso Hasi, Kuwa Nje Ya Rekodi na Kuwa Kwenye Rekodi.

### 4.3 Vijana na wazazi wao

Mikakati inayobainika kati ya vijana na wazazi wao ni ya mseto lakini kama vile inavyodhihirika ni kuwa mikakati inayowakilishwa na nambari 1, 3, 4 katika sura ya tatu; yaani, **kuwa kwenye rekodi, upole hasi na kuwa nje ya rekodi** inasheheni matumizi ya lugha ya vijana kati yao na wazazi wao. Asilimia 50% ya vijana wa kiume walitokea kutumia Upole Hasi katika mwingiliano wao na wazazi wao, hii ikiangazia maswala yote yaliyoangaziwa katika utafiti ikilinganishwa na asilimia 50.41% ya vijana wa kike waliotumia Upole Hasi. Kuwa Kwenye Rekodi baina ya vijana wa kiume kulitokea kuwa na asilimia 39.3% nao wasichana 45.7%. Kuwa Nje Ya Rekodi kulidhihirisha asilimia 37.04% ikilinganishwa na wasichana ambao walikuwa na asilimia 39.16%. Utafiti ulibainisha kuwa vijana wa kiume wanapenda kukwepa Tendo La Kutishia Uso hasa ikiwa linamuhusu mzazi wake, mfano swala la hedhi asilimia 26.7% ilijizuia na kusema mambo kama haya ;

*Nitajifanya sijaona kisha nitoweke.*

Vijana wengine hawakukamilisha sehemu hiyo, kukosa kujaliza sehemu hiyo bila shaka kunadhihirisha kuwa vijana huwa makini wanapoitumia lugha; hata hivyo jambo la kushangaza ni kuwa asilimia 20% ya vijana wa kiume ilikabiliana na swala la hedhi kwa njia ya moja kwa moja ikilinganishwa na kundi la kike.

Kwa mfano;

*Hey mam kuna damu kwa nguo yako...*

*Mbona unatokwa na damu.*

Upole Hasi ulitokea kudhaminiwa sana na makundi yote mawili pale swala la kupigiwa simu na mchumba wa siri lilitakiwa kuelezewa ni nani aliyepiga. Yanayoibuka hapa ni madanganyo ya upole. Japo mzazi huenda akajua alidanganywa, ukweli ni kuwa uso wake Hasi hautakuwa umedhuriwa, asilimia 100% kwa vijana wote ilidhihirika. Mkakati wa uongo ni njia moja ambayo vijana hutumia kama njia ya kudhihirisha upole. Dhihirisho la matokeo ya wasichana kutumia kiwango cha juu cha mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi dhidi ya wazazi wao ni dhihirisho kuwa wasichana wanao mwingiliano wa karibu sana na wazazi wao zaidi ya vijana wa kiume.

Swala la vijana kuwa wamekasirishwa na uwezekano wa kutoa tusi kwa wazazi wao limedhihirisha kuwa wavulana wanaweza kuwatusi wazazi wao kwani asilimia 40% yao walitumia mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi. Wasichana kwa upande wao walikuwa asilimia20%.

Baadhi ya matusi ni kama vile;

*Shit!!*

Mjinga,

Mjinga wewe,

Ungenia*bort*,

*You spoilt brat,*

Nyinyi ni wajinga sana niacheni,

Vijana wengine walidhihirisha kukerwa kwao kwa kuyatumia maneno ambayo yalisheheni uchungu. Vihisishi vilitumiwa vile vile,

Kwa mfano;

*Daaad!*

Wewe ndiye unanianzanga tu,

Unaniboo,

'Kwenda' ni neno ambalo limetokea kutumiwa na wengi, bila shaka huenda linaeleweka kama njia moja ya kudhihirisha kubughudhiwa kwa vijana na wazazi wao na watu wengine kwa jumla.

Tukio lingine ambalo linadhihirisha kuwa wavulana huitumia lugha yao kiholela ni pale ambapo wanampata mama yao akiwa amekaa vibaya, linalodhihirika hapa ni kuwa asilimia 60% ya wasichana dhidi ya asilimia 40% ya wavulana inawasuta moja kwa moja na kuwambia maneno kama haya;

*Sit well*

Funika

Hiyo nguo yako inaonekana,

Funika uchi mama,

Mama umekaa vibaya,

Kundi lingine liliegemea mkakati wa Kuwa Nje Ya Rekodi, ambapo maelezo kama haya yalitumiwa.

Tengeneza hiyo nguo yako,

Kuja nikwambie jambo kwa nyumba,

*Am sure you don't wonna embarrass yourself,*

Mam amka hapo chini kuna nyoka, n. k

*UFUNGUO*

A-Methali

B-Uvutaji wa sigara

C-Swala la hedhi

D-Swala la maliwato

E-Swala la fedha

F-Swala la kuchumbiana

G-Mgonjwa wa UKIMWI

H- Swala la mapenzi yenye ila

I-Swala la zipu

J-Swala la tanzia

K-Swala la wizi

L-Swala la kujamiiana

M-Swala la kushuta

N-Swala la simu ya mchumba

O-Swala la mkao mbaya

P-Swala la njia na dharura

Q-Swala la ubakaji

R-Swala la kunya pasipofaa

S-Swala la jina la sehemu za siri

T-Swa la kutusi

Wtf-(wavulana 15, wasichana,15) = watafitiwa 30

Jedwali la 11

Wavulana na wazazi wao

| mkt | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | | | | | | | | | | |
| B | 9 | 60 | | | 5 | 33.3 | 1 | 6.7 | | |
| C | 3 | 20 | 1 | 6.7 | | | 7 | 46.7 | 4 | 26.7 |
| D | 8 | 53.3 | | | 3 | 20 | 4 | 26.7 | | |
| E | 3 | 20 | 1 | 6.7 | 11 | 73.3 | | | | |
| J | 11 | 73.3 | | | 1 | 6.7 | 3 | 20 | | |
| M | | | | | 13 | 86.7 | 2 | 13.3 | | |
| N | | | | | 15 | 100 | | | | |
| O | 9 | 60 | | | | | 6 | 40 | | |
| P | 3 | 20 | 1 | 6.7 | 11 | 73.3 | | | | |
| R | 6 | 40 | | | 1 | 6.7 | 5 | 33.3 | 3 | 20 |
| S | 1 | 6.7 | | | | | 13 | 86.7 | 1 | 6.7 |
| T | 6 | 40 | | | | | 9 | 60 | | |
| jml | | 39.3% | | 6.7% | | 50% | | 37.04% | | 17.8% |

*UFUNGUO*

1 - Kuwa kwenye rekodi (mkakati unaoyasema mambo kama yalivyo).

2 -Upole chanya (mkakati unaozuia mgongano, uwepo wa urafiki, umoja).

3 -Upole hasi (njia za kudhihirisha uhuru kwa msikilizaji).

4 -Kuwa nje ya rekodi (mkakati usiokuwa wa moja kwa moja).

5 -Hazijatumia lugha safi, yenye adabu na kadhalika.

6 - Hazieleweki.

*Kutofanya Tendo La Kutishia Uso

Jedwali la 12

Wasichana na wazazi wao

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | 10 | 66.7 | | | 5 | 33.3 | | | | |
| C | 2 | 13.3 | | | 11 | 73.3 | 2 | 13.3 | | |
| D | 12 | 80 | | | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | | |
| E | 1 | 6.7 | 1 | 6.7 | 13 | 80.7 | | | | |
| J | 13 | 86.7 | | | | | 2 | 13.3 | | |
| M | | | | | 9 | 60 | 6 | 40 | | |
| N | | | | | 15 | 100 | | | | |
| O | 6 | 40 | | | 3 | 20 | 6 | 40 | | |
| P | 8 | 53.3 | | | 7 | 46.7 | | | | |
| R | | | | | 4 | 26.7 | 9 | 60 | 2 | 13.3 |
| S | | | | | | | 15 | 100 | | |
| T | 3 | 20 | | | | | 12 | 80 | | |
| jml | | 45.7% | | 6.7% | | 50.43 % | | 39.16 % | | 13.3% |

## 4.4 Vijana na walimu wao

Mwingiliano wa vijana na walimu wao unadhihirisha uwepo wa mseto wa mikakati ya upole ya matumizi ya lugha ya vijana, asilimia kubwa ya wavulana ilitokea kuyasema mambo kama vile yalivyo, hili ni dhihirisho la kundi hili kukosa simile katika matumizi yao ya lugha kwani baadhi ya maswala yalikuwa ya kuzua mihemko.

Kwa mfano;

*Hey teacher* alifariki jana usiku.

Nimepata habari kuwa nani amekufa.

Amekufa.

Funga zipu.

Mwalimu hujafunga zipu.

Funika uchi mwalimu.

Swala la wizi nalo lilitokea kukabilianwa nalo pasina haja ya kuepuka Tendo La Kutishia uso kwani asilimia ya wavulana ilikuwa 80% nao wasichana73.3%, haya yanatokea kuelezewa na ukweli kuwa mhusika alikuwa mmoja wao na hawakuwa na haja ya kuunusuru uso wake kwani walikuwa wamehasiriwa na vitendo vyake. Kwa ufupi wasichana wamedhihirisha kuwa wanaudhamini upole zaidi ya wavulana kwani asilimia za namna wanavyotekeleza mikakati yao imesheheniwa na upole ikilinganishwa na wavulana. Wavulana walitokea kuitumia mikakati ya Upole Hasi na Kuwa Nje ya Rekodi kwa kiwango cha chini dhidi ya walimu wao, tukio hili linadhihirisha dhana ya ubabe walionao wavulana, asilimia 41.34% ya Kuwa Kwenye Rekodi dhidi ya 34.45% ya wasichana inadhihirisha hili.

Jedwali la 13

Wavulana na walimu wao

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | 8 | 53.3 | | | 3 | 20 | 3 | 20 | 1 | 6.7 |
| D | 4 | 26.7 | | | 11 | 73.3 | | | | |
| G | 8 | 53.3 | 2 | 13.3 | 3 | 20 | 2 | 13.3 | | |
| H | 3 | 20 | | | 3 | 20 | 8 | 53.3 | 1 | 6.7 |
| I | 7 | 46.7 | | | 4 | 26.7 | 4 | 26.7 | | |
| J | 12 | 80 | | | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | | |
| K | 12 | 80 | | | | | 3 | 20 | | |
| L | 6 | 40 | | | 2 | 13.3 | 6 | 40 | 1 | 6.7 |
| M | | | | | 13 | 86.7 | 2 | 13.3 | | |
| P | 1 | 6.7 | | | 14 | 93.3 | | | | |
| S | 1 | 6.7 | | | | | 13 | 86.7 | 1 | 6.7 |
| jml | | 41.34 % | | 13.3% | | 40.73 % | | 33.33 % | | 6.7 % |

Jedwali la 14

Wasichana na walimu wao

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | | | 2 | 13.3 | 8 | 53.3 | 5 | 33.3 | | |
| D | | | | | 13 | 86.7 | 2 | 13.3 | | |
| G | 1 | 6.7 | 2 | 13.3 | 2 | 13.3 | 9 | 60 | 1 | 6.7 |
| H | | | | | 1 | 6.7 | 14 | 93.3 | | |
| I | 3 | 20 | | | 11 | 73.3 | 1 | 6.7 | | |
| J | 8 | 53.3 | | | 1 | 6.7 | 6 | 40 | | |
| K | 11 | 73.3 | | | 1 | 6.7 | 3 | 20 | | |
| L | 7 | 46.7 | | | | | 8 | 53.3 | | |
| M | | | | | 14 | 93.3 | 1 | 6.7 | | |
| P | 1 | 6.7 | | | 14 | 93.3 | | | | |
| S | | | | | | | 15 | 100 | | |
| jml | | 34.45 % | | 13.3% | | 48.14 % | | 42.66 % | | 6.7 % |

## 4.5 Vijana na marafiki zao

Matumizi ya lugha hutawaliwa na wahusika wanaoshiriki mazungumzo, pamoja na uhusiano wao. Ipara na Maina (2008:66) wameangazia kuwa mazungumzo ya maharimu yatasheheni matumizi ya lugha yenye utani, mzaha au maneno yenye ukali ilhali wahusika hawatiani makonde bali ni kuchangamka. Ukweli huu umedhihirika bayana kwani tukio la vijana kutumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi kunadhihirisha uhuru walio nao dhidi ya mwingine pale mawasiliano yanawahusu.

Kwa mfano; (swala la 'kuchafua hewa')

*Ha! Ha! Ha! Let's assume it never happened.*

Iza mtu kameponyoka.

Vumilia kidogo hiyo ni hali ya afya.

Napunguza ma*steem* manze usijali.

n. k.

Pale ambapo jambo fulani linasawiri picha mbaya zaidi vijana walitokea kutumia mkakati wa Kuwa Nje Ya Rekodi.

Kwa mfano; swala la hedhi

Naona kuna shida naweza kusaidia?

*What's up with your skirt?*

Hukujitayarisha vizuri

Afrika imejichora kwa nguo

Funga sweta nyuma yako

Asilimia kubwa ya wavulana idhihirisha chembechembe ya kutawaliwa na upole zaidi ya wasichana ambao walidhihirisha matumizi mengi ya Kuwa Kwenye Rekodi. Yumkini huu ni utani uliongaziwa na Ipara na Maina (k.h.j)

*Beste* yako amekuwa 'Matheri'.

Yule *boy* ana *groove* na boy mwenye anakula vitu.

Manze *gas* imenijaa wacha niitoe

Swala la kukaa vibaya lilizua matokeo ya kuwepo na utani,

Kwa mfano;

Funga duka

Yenyewe funga duka

Kwani mali yako ni ya jamii? *Watch it!*

Swala la uwezekano wa kutusi linaakisi namna vijana walivyo wepesi wa kubwaga matusi kwa wenzao kwani asilimia 86.7% ya wavulana dhidi ya 100% ya wasichana iliyatoa matusi kwa wenzao moja kwa moja. Mfano; (wsichana)

Kwenda huko mbwa wewe,

Fala,

Kumbafu,

Kuku wewe,

*Stupid fool*

*Asshole,*

Gasia,

n. k

Kwa kifupi, vijana wamedhihirika kuwa wepesi katika kuyatoa matusi kwa wenzao. Swala la jina badalia la kutajia sehemu za siri lilidhihirisha kuwa wasichana hawapendi kuzitaja ovyo ovyo sehemu za siri kwa kulitumia jina moja lakini walipendelea kuutumia mkakati wa Kuwa Nje Ya Rekodi kwani asilimia 100% ya wasichana dhidi 80% ya wavulana ilibainisha matumizi ya lugha ya mzunguko. Wasichana walitumia kwa wingi vishazi kama;

*Madwale zinachura,*

*My* ninino *is paining,*

Nimeumia mahali pabaya,

Haki nimeumia kwa mmh!

Nimeumia sehemu nyeti,

n. k.

Vijana wamedhihirisha matumizi ya Utafutaji wa Fadhila hasa pale wanapotaka haja zao zikidhiwe na marafiki zao, wazazi wao, watu wasiofahamiana nao n. k, utafiti huu ulibainisha kuwa mbinu za kutanguliza maongezi katika harakati za kutafuta 'urafiki' wa jinsia tofauti huanza kwa maneno kama haya;

Sasa,

Niaje,

Manze,

*Excuse,*

Hi ningependa...

Unaweza *spare,*

n. k.

Huu ni utafutaji wa fadhila ambao unaendana na mkakati wa Upole Hasi.

Jedwali la 15

Wavulana na marafiki zao

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | 14 | 93.3 | | | | | 1 | 6.7 | | |
| C | 1 | 6.7 | 2 | 13.3 | | | 11 | 73.3 | 1 | 6.7 |
| D | 11 | 73.3 | | | | | 4 | 26.7 | | |
| E | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | 12 | 80 | | | | |
| F | | | | | 15 | 100 | | | | |
| G | 9 | 60 | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | 3 | 20 | | |
| H | 8 | 53.3 | | | | | 7 | 46.7 | | |
| I | 13 | 86.7 | | | 1 | 6.7 | 1 | 6.7 | | |
| J | 11 | 73.3 | | | | | 4 | 26.7 | | |
| K | 13 | 86.7 | 1 | 6.7 | | | 4 | 26.7 | | |
| L | 8 | 53.3 | 1 | 6.7 | | | 4 | 26.7 | 2 | 13.3 |
| M | 1 | 6.7 | 1 | 6.7 | 1 | 6.7 | 12 | 80 | | |
| P | 9 | 60 | | | 4 | 26.7 | 2 | 13.3 | | |
| Q | 12 | 80 | | | | | 3 | 20 | | |
| R | 12 | 80 | | | | | 3 | 20 | | |
| S | 3 | 20 | | | | | 12 | 80 | | |
| T | 13 | 86.7 | | | | | 2 | 13.3 | | |
| jml | | 58.33% | | 8.9% | | 37.8% | | 31.12% | | 10.0% |

Jedwali la 16

Wasichana na marafiki zao

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | 12 | 80 | | | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | | |
| C | 3 | 20 | | | 4 | 26.7 | 8 | 53.3 | | |
| D | 15 | 100 | | | | | | | | |
| E | 3 | 20 | 5 | 30 | 7 | 46.7 | | | | |
| F | 1 | 6.7 | | | 14 | 93.3 | | | | |
| G | 12 | 80 | 1 | | 1 | 6.7 | 1 | 6.7 | | |
| H | 6 | 40 | | | 1 | 6.7 | 8 | 53.3 | | |
| I | 13 | 86.7 | | | | | 2 | 13.3 | | |
| J | 13 | 86.7 | 1 | 6.7 | | | 1 | 6.7 | | |
| K | 12 | 80 | | | | | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 |
| L | 8 | 53.3 | 1 | | | | 6 | 40 | | |
| M | 6 | 40 | 1 | 6.7 | 4 | 26.7 | 4 | 26.7 | | |
| P | 9 | 60 | 1 | 6.7 | 4 | 26.7 | 1 | 6.7 | | |
| Q | 12 | 80 | | | | | 3 | 20 | | |
| R | 12 | 80 | | | 1 | 6.7 | 2 | 13.3 | | |
| S | | | | | | | 15 | 100 | | |
| T | 15 | 100 | | | | | | | | |
| jml | | 63.34 % | | 10.58 % | | 26.68 % | | 28.89% | | 6.7% |

## 4.6 Vijana na watu wasiowajua

Mawasiliano baina ya vijana na watu wasiofahamiana nao hutokea kumwelekeza mtu kuchagua mkakati unaofaa, jambo la kimsingi hapa ni kuwa uchaguzi utaegemea ukweli kuwa msemaji na msikilizaji wanazungumzia nini. Ikiwa kijana atakuwa ameudhiwa,

ataegemea mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi lakini akiwa ana uhitaji wa kitu basi atautumia mkakati wa Upole Hasi au Kuwa Nje Ya Rekodi. Utafiti wetu ulibainisha hayo. Vijana wa kiume na wa kike walitokea kuwa na asilimia100% mtawalia walipokuwa wana uhitaji wa pesa. Maneno waliyosema ni kama vile;

Ni aje? Nilikuwa naomba *doo* kiasi tu, si uni*help*...,

*Excuse,* uko na *fifty bob* unisaidie tafadhali?

Tafadhali nisaidie na pesa kadhaa kwani nimekwama *place* fulani

Nimepatwa na janga na naomba msaada wa hela chache tu,

n.k

Hapa vijana hawa wanatumia mbinu kabambe za kumshawishi mtu huyo wasiyefahamiana naye ili kupata ufadhili. Tukio hili ni tofauti na pale vijana wanatokea kubughudhiwa na watu hao ambapo mkakati unabadilika na kuwapelekea vijana kuutumia mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi. Swala la kunya mahali pasipofaa kunapelekea vijana kuwakabili watu hao kwa maneno kama haya;

Leo utanijua poa,

*Are you mad?* Unafikiria *this is a public toilet.*

Wewe wacha kunya hapo.

*Grow up silly!*

Wacha ujinga zako sura mbaya,

n.k

Asilimia hapa ni 66.7% ya wavulana dhidi 60% ya wasichana mazungumzo yao yalijikita katika mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi. Wasichana na wavulana wanatokea kubainisha uwepo wa tofauti kwani wasichana wanadhihirisha matumizi ya Upole Hasi ambapo kiwango chao ni dhihirisho la upole, yaani wanawajali watu hao zaidi ya wavulana. Matusi yanayotokea kuelekezewa watu hawa yanadhihirsha kuwa vijana wa kiume ni wepesi wa kutusi kwani asilimia 60% dhidi ya 33.3% ya wasichana ilitokea kuwatusi watu hawa bila kuijali hadhi, umri, na tukio lililopelekea wao kufanya hivyo. Matusi yaliyotolewa ni kama haya;

Mkongwe asiyejielewa,

Mwehu tena mjinga,

Muone huyu wazimu,

Shenzi wewe

*Bull shit!*

Mkakati utabadilika pindi pale vijana wanapotaka kusaidiwa kwa njia moja au nyingine.

Jedwali la 17

Wavulana na watu wasiowajua

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | 8 | 53.3 | | | 4 | 26.7 | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 |
| C | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | | | 8 | 53.3 | 4 | 26.7 |
| E | | | | | 15 | 100 | | | | |
| J | 7 | 46.7 | | | 3 | 20 | 5 | 33.3 | | |
| P | 4 | 26.7 | | | 11 | 73.3 | | | | |
| R | 10 | 66.7 | | | 2 | 13.3 | 3 | 20 | | |
| T | 9 | 60 | | | | | 6 | 40 | | |
| jml | | 44.45 % | | 6.7 % | | 46.66 % | | 28.38 % | | 16.7% |

Jedwali la 18

Wasichana na watu wasiowajua

| wtf | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | 2 | 13.3 | 1 | 6.7 | 10 | 66.7 | 2 | 13.3 | | |
| C | | | | | 7 | 46.7 | 8 | 53.3 | | |
| E | | | | | 15 | 100 | | | | |
| J | | | | | 14 | 93.3 | 1 | 6.7 | | |
| P | 14 | 93.3 | | | | | 1 | 6.7 | | |
| R | 9 | 60 | 1 | 6.7 | 3 | 20 | 1 | 6.7 | 1 | 6.7 |
| T | 5 | 33.3 | | | | | 10 | 66.7 | | |
| jml | | 35.53% | | 6.7% | | 65.3% | | 25.56% | | 6.7% |

## 4.7 Vijana na watoto wadogo, mgonjwa na daktari

Mielekeo ya vijana katika matumizi ya lugha ilitokea kutofautiana sana kwa kuegemea tukio na umri pale wahusika walikuwa watoto wadogo, mgonjwa wa UKIMWI na daktari.

Kwa mfano:

Tukio lolote lililokuwa likimzungukia mtoto lilitokea kudhihirisha matumizi ya mkakati wa Kuwa Kwenya Rekodi. Jambo lililopelekea matokeo kudhihirisha kuonewa kwa watoto na vijana hata pale wametokea kulifanya jambo la kuudhi kama vile 'kuchafua hewa', waliwasingizia watoto hao. Asilimia 60% ya wavulana dhidi ya asilimia 40% ya wasichana walilikabili swala hilo nyeti moja kwa moja.

> Ni kwa nini umejamba?
>
> We... tabia mbaya,
>
> Wewe wacha tabia mbaya,
>
> We unafanya nini ...toka nje.
>
> Umko! Hata hauna adabu.
>
> Pelekesha udaku kwenyu
>
> Ah! Hiyo ni tabia mbaya usifanye hivyo mbele ya watu.

Hata hivyo, madanganyo ya upole yalitokea kusheheni namna vijana walivyokabiliana na hali hiyo;

Kwa mfano;

> Kwani kuna paka hapa anakoroma?
>
> Wewe wacha ni tumbo *imeghuruma*
>
> Pole usifanye hivyo!
>
> Ardhi ni kutetemeka inatetemeka.

Gari ya moshi imepita.

Watoto walitokea kubwagiwa matusi pasina simile kwani mkakati uliotumiwa ni ule wa Kuwa Kwenye Rekodi, wavulana pamwe na wasichana walidhihirisha asilimia 100%, matusi kama haya yalitolewa;

Mjinga we,

Kichwa kubwa,

Shetani msalabani, una pepo punda!

Matako ya mama yako.

Umbwa wewe,

Malaya wewe,

*Stupid! Go away brare fuckin* mjinga wewe?

n.k

Watoto hawakutokea kuelezewa waziwazi mahali vijana walikuwa wameumia, asilimia100% kwa upande wa wasichana pamwe na wavulana ilitokea kudhihirisha matumizi ya lugha ya mzunguko ili kuashiria maelezo ya sehemu nyeti. Kwa ufupi, swala lolote nyeti lililotokea kumdhalilisha kijana fulani lilikabilianwa nalo kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Hasa pale wanapoambiwa kutaja jina la sehemu za siri ikiwa ameumia. Njia za mzunguko kama hizi zilitumiwa,

Jamani nimeumia huku *down,*

Nimeumia *down* chini,

Naumwa nikienda kukojoa,

Nimeumia mahali pabaya,

Nimeumia mahali hapasemeki kwa umati,

Nimeumia katikati ya miguu,

*My 'ninino' is paining,*

Nimeumia *place* zingine *painful,*

Naumia huko,

Hizo *parts* hazi*feel* poa,

Nimeumia sehemu nyeti,

n. k.

Mkakati wa Upole Hasi ulitokea kutumiwa na vijana pale swala la mtu mgonjwa wa UKIMWI lilitokea kuangaziwa. Asilimia 73.3% ya wavulana ilibainika dhidi ya asilimia 86.7% ya wasichana; hili lilikuwa dhihirisho la kuwepo na imani dhidi ya wahasiriwa wa ugonjwa huu. Lugha iliyotumika ilisheheni maneno kama;

Usife moyo,

Fuata maagizo ya daktari utapona hivi karibuni,

Umeanza kujenga,

Pole kwa ugonjwa, lakini leo yaonekana umepata nguvu

Utapona hivi karibuni, pole sana!

*Don't worry*! Kuna *masurvivors!*

Wa! Umeendelea vyema sana

Tukio la vijana kutumia mkakati wa Kuwa Nje Ya Rekodi ili kumwelezea daktari kuwa walikuwa wameumia sehemu nyeti ni dhihirisho tosha kuwa maswala yanayowagusa na yawe ya kukirihisha, yanazua matumizi ya njia za mzunguko, asilimia 80% ya wavulana dhidi *ya* 100% *ya* wasichana ilitokea kuutumia mkakati huu. Lililotakiwa hapa ni kutajwa kwa jina moja ambalo wangeweza kulitajia sehemu hiyo nyeti.

Jedwali la 19

Wavulana na watoto wadogo kushuta, kunya, kutusi, jina la sehemu za siri / mgonjwa wa ukimwi / mgeni na sigara / daktari na sehemu za siri

| wtf | *mhusika* | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | *mgeni* | 4 | 26.7% | | | 8 | 53.3% | 3 | 20 | | |
| G | *mhasiriwa* | | | 4 | 26.7% | 11 | 73.3% | | | | |
| M | *mtoto* | | | | | 5 | 33.3 | 9 | 60 | * | 6.7 |
| S | *mtoto* | | | | | | | 15 | 100 | | |
| R | *mtoto* | 12 | 80 | | | | | 3 | 20 | | |
| T | *mtoto* | 15 | 100 | | | | | | | | |
| *jml* | | | 90% | | | | 33.3% | | 60% | | 6.7% |
| S | *daktari* | 3 | 20% | | | | | 12 | 80% | | |

Jedwali la 20

Wasichana na watoto wadogo kushuta, kunya, kutusi, jina la sehemu za siri / mgonjwa wa ukimwi / mgeni na sigara / daktari na sehemu za siri

| wtf | *mhusika* | 1 | % | 2 | % | 3 | % | 4 | % | * | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | *mgeni* | 3 | 20% | 1 | 6.7% | 11 | 73.3% | | | | |
| G | *mhasiriwa* | 1 | 6.7% | 2 | 13.3% | 12 | 86.7% | | | | |
| M | *mtoto* | 3 | 20% | 1 | 6.7% | 4 | 26.7% | 6 | 40% | 1 | 6.7% |
| S | *mtoto* | | | | | | | 15 | 100% | | |
| R | *mtoto* | 14 | 93.3% | 1 | 6.7% | | | | | | |
| T | *mtoto* | 15 | 100% | | | | | | | | |
| *jml* | | | *71.1%* | | 6.7% | | 26.7% | | *70%* | | 6.7% |
| S | *daktari* | | | | | | | 15 | 100% | | |

## 4.8 Hitimisho

Sura hii imedhihirisha kupitia uchanganuzi kuwa mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana inatofautiana kutoka mkakati mmoja hadi mwingine kwani matokeo haya yanaegemea tukio, wahusika, kusudi la kuelezea jambo fulani na kadhalika. Uchanganuzi huu umetambulisha na kudhibitisha kuwepo kwa mikakati kadhaa ambayo vijana huitumia, tofauti kati ya matumizi ya mikakati ya upole baina ya wasichana na wavulana imesawiriwa bayana. Vijana wamedhihirisha kuwa inapotokea kuwe na mtagusano na kikundi fulani katika jamii ni muhimu kwa kila mshiriki kuunusuru uso wake au hata kujaribu kutolifanya Tendo la Kutishia Uso wa mwingine.

# SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho inaangazia kwa kifupi muhtasari wa matokeo, mapendekezo, mipaka ya utafiti na kutoa rai kwa utafiti zaidi wa baadaye.

## 5.2 Muhtasari wa matokeo

Utafiti huu ulikuwa juu ya uchanganuzi wa kipragmatiki katika lugha ulioegemea kutambulisha mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana. Utafiti wenyewe ulijikita kikamilifu katika Nadharia Ya Upole ya Brown na Levinson (1987) ambayo imeimarishwa kutoka kwa Nadharia yake Ervin Goffman ya 'Uso' inayohusika na mtagusano wa binadamu na ambapo tunaelezwa kwa yakini kwa nini binadamu husitiri uso wake na kuusitiri vile vile wa mtu mwingine. Utafiti wetu uliongozwa na maswali haya na mengine;

- Je vijana hutumia mikakati gani katika matumizi ya lugha yao?
- Je lugha ya vijana ina upole au la?
- Je lugha ya vijana hudhihirisha upungufu wa nidhamu?
- Je kati ya wavulana na wasichana ni kikundi gani ambacho hudhihirisha upole zaidi katika matumizi ya lugha?

Kutokana na data tuliokusanya na matokeo ya uchanganuzi, tulibainisha bayana kuwa vijana hutumia mseto wa mikakati ya upole katika matumizi ya lugha. Kunao ushahidi vile vile wenye mashiko kuwa mikakati hutegemea vijana wanawasiliana na nani, mada ni gani, sababu za kuwasiliana ni gani n. k.

Utafiti huu uliweza kutambulisha kuwa vijana hutumia mikakati kama vile Kuwa Kwenye Rekodi, Upole Hasi, Upole Chanya, Kuwa Nje Ya Rekodi na Kutolifanya Tendo La Kutishia Uso. Tofauti ya matumizi ya mikakati hii ilibainika kwani Kuwa Kwenye Rekodi, Upole Hasi na Kuwa Nje Ya Rekodi kulitokea kutumiwa sana. Jambo la kimsingi lililodhihirika ni kuwa, ilitegemea mzungumzaji na msikilizaji ni nani. Ushahidi huu unaipa nadharia yetu tete ya tatu msingi kuwa; vijana hutumia mikakati ya lugha kusafidi habari nyeti katika matumizi yao ya lugha wanapowasiliana.

Utafiti wetu uliweza kubainisha kuwa kuna matumizi safidi ya lugha katika mazungumzo ya vijana; ukweli uliodhihirika hapa ni kuwa mikakati hii ya kuisafidi lugha ilitegemea uhusiano wa vijana na hadhira yao, umri, mada na sababu za mawasiliano. Tulibainisha kuwa watoto wadogo wanasutwa bila ya kujali kuzitishia nyuso zao kwani kama ni kutusiwa, walitusiwa pasina kuwa na simile. Walipotaka faida iwaendee wao, mkakati ulikuwa ule wa kushawishi; mfano mzuri ni pale wanapotaka kuibua njia ya kuanza harakati za kuchumbiana; vijana walitokea kuutumia mkakati wa Upole Hasi ambao kulingana nao Brown na Levinson waliuita Utafutaji wa Fadhila, kwani maneno kama ***sasa, niaje, tafadhali,*** n. k. yalitokea kutanguliza maongezi.

Ufumbuzi mwingine tulioibua ni kuwa nidhamu katika matumizi ya lugha ya vijana hudhihirisha kiwango fulani cha utovu wa adabu ambapo tokeo hili hutegemea tukio la mawasiliano, hadhira na jinsia. Nidhamu, mfano wa asilimia 100% inatokea tu pale vijana

wanataka wakidhiwe haja zao kinyume na pale ambapo wameudhiwa ambapo utovu wa adabu utatokea kudhihirika. Jambo lingine tulilobainisha ni kuwa vijana wa kike walitokea kudhihirisha upole zaidi ya vijana wa kiume.

## 5.3 Mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulitokea kutambua kuwa matumizi ya hojaji huenda yakawa magumu kwani watafiti huenda wasiyajibu maswali yote hasa kama kuna yale yanatokea kuzua mihemko zaidi. Watafitiwa wengine walitokea kuyajibu maswali kwa njia ya usemi taarifa katika utafiti wetu wa kimajaribio kinyume na usemi halisi; kwa sababu hii ilitubidi kuwaongoza watafitiwa kabla ya kuanza kuyajibu maswali.

Katika shule nilizokwenda watafitiwa wengi na walimu wao waliingiwa na kimako kuhusiana na maswala ya utafiti, hawakuweza kuona kwa nini nilikuwa nimeamua kuufanya utafiti kama huo kwani kulingana nao ulikuwa unakirihisha.

Utafiti huu ni hatua nzuri kuelekea mtazamo chanya kuhusiana na matumizi ya lugha ya vijana, kwani kuwaelewa kutapelekea kukabiliana na maswala kikamilifu ikiwa jambo fulani litatakiwa kuwafikia vijana. Swala la muda lilikuwa pingamizi kwani kazi nyingi niliifanyia mbali na Chuo Kikuu, hivyo basi ilinibidi kuhakikisha kuwa ninakabiliana na hali ngumu huko mashinani.

## 5.4 Rai kwa utafiti zaidi

Utafiti huu ulijikita katika ukusanyaji wa data kwa kutumia hojaji ili kubainisha uwepo wa mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana, hili tulilifanya lakini kitu kimoja ambacho ningependekeza ni kuwa kama utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa njia ambayo vijana hawajui kuwa wanafanyiwa utafiti, huenda matokea yetu yakapata msukumo na kubainisha kwa yakini kuwa vijana wanayo mikakati mseto ya upole katika matumizi yao ya lugha.

MAREJELEO

Brown, P. and S. Levinson (1987) *Politeness: Some universals in language usage.* Cambridge: Cambridge University Press.

Buliba, A, Njogu, K na Mwihaki, A (2006) *Isimujamii kwa wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Carter, R and McCarthy,M (1994) *Language and discourse – perspective for Language Teaching.* New York. Longman Publishing,

Crystal, D.*(2000). Language Death.* New York: Cambridge University *Press.*

Eastman, C. M. (1990). *Aspects of Language and Culture*. Novato: Chandler & Sharp Publishers, Inc.

Elhadad, M, (1991) Generating Adjectives to Express the Speaker's Argumentative Intent. In Proceedings of the Fifth National Conference on Artificial Intelligence (AAAI-91), pages98-104, 1991.

Fromkin, V. Rodman, R (1988) *Introduction to Language.* Holt: Rinechart and Winston.

Fromkin, V. Rodman, R. and Hymes, N. (2003) *An Introduction to Language. (7th Ed)* Boston: Wardsworth Thompson Corporation.

Grice, H. P. (1975)*"Logic and conversation," Syntax and Semantics 3: Speech Acts*, Cole, P. & Morgan, J. L. (eds.), New York: Academic Press.

Hofmann, R (1993) *Realms of Meaning, an introduction to semantics*. London: Longman.

Hovy, H. E (1988) *Generating Natural Language Under Pragmatic Constraints*. Lawrence Erlbaum, Hillsdale, N J.

Hudson (1995*). Language and Society.* London: Macmillan Publishers.

Igboanusi, H. (2001) *LanguageAttitude and Language Conflicts in West Africa*. Ibadan: Enicrowfit Publishers.

Ipara, I.O na Maina, G (2008) *Fani ya Isimujamii kwa shule za sekondari.* Nairobi: Oxford University Press.

King'ei .K na Kobia .J (2007) *Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini Kenya. Nordic Journal of African Studies* 16(3): 320 – 332 Kenya.

Lakoff, R (1973) *The Logic Of Politeness; or minding your p's and q's*. Paper from the 9th Regional Meeting, Chicago Linguistics Society. Chicago: Chicago Linguistics Society. Universitas Mataram.

———. (1977). "*What You Can Do With Words: Politeness, Pragmatics, and Performatives*." In Rogers, Wall and Murphy (1977), 79-105.

Lakoff, G. and Johnson, M. (1980) *Metaphors We Live By.* University of Chicago Press.

Leech, G. (1983) *Principles Of Pragmatics*. Singapore: Longman Publishers.

Leech, G. (1986) *Automatic Grammatical Analysis And Its Educational Applications*, in Leech and Candlin pp206-219.

Levinson, S. (1983) *Pragmatics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Mahyuni (2008) *The Socio-Cultural Significance Of Valuing Linguistic Politeness*: Theoretical Frameworks Vol. 15. No. 28 Maret 2008-06-19 128 SK Akreditasi Nomor: 007/BAN PT/Ak-V/S2/VIII/2006

Marcus, M (1987) *Generation Systems Should Choose Their Words*. In Yorick Wilks, editor, Theoretical Issues in Natural Language Processing, pages 211-214. New Mexico State University, Las Cruces.

Mbaya. M (2002) *Linguistic Taboo In African Marriage Context: A Study Of The Oromo Laguu. Nordic Journal of African Studies* 11(2): 224-235 Senegal: University of Gaston Berger.

McDonald, D (1991) On the Place of Words in the Generation Process. In C. L.

Mills, S. (2003) *Gender and politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.

Msanjila Y.P. (2007) Utumiaji Wa Kiswahili Na Lugha Za Jamii Kijinsia Nchini Tanzania. *Nordic Journal of African Studies* 16(1):18-29 university of Dar es Salaam Tanzania

Nirenburg, S and Nirenburg I, (1988) *A Framework for Lexical Selection in Natural Language Generation*. In Proceedings of the 12th International Conference on Computational Linguistics (COLING-88), pages 471-475, Budapest, 1988.

Njeri,S (2007) A pragmatic Analysis of Gikuyu Lexical euphemisms in HIV/AIDS Discourse. Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa, University of Nairobi.

Ongechi, N.O. (2002) Trilingual Code switching In Kenya: Evidence From Ekegusii, Kiswahili, English, And Sheng. Unpublished Ph D Thesis. Hamburg: University of Hamburg.

Rayson, P., Leech, G. , & Hodges, M. (1997). *Social differentiation in the use of English vocabulary:* Some analyses of the conversational component of the British National Corpus. *International Journal of Corpus Linguistics, 2 (1)*, 133-152.

Stanford Encyclopedia of Philosophy (2005)
(htt:// plato Stanford. edu/ entries/implicature)

Stenstrom, A.B. (1999). He was really gormless-she's bloody crap. Girls, boys and intensifiers. In H. Hasselgard and S. Oksefjell (eds) Out of Corpora: Studies in Honor of Stig Johansson (pp. 69-78). Amsterdam: Rodopi.

Tannen, D. (1984) *Conversational Style: Analyzing Talk Among Friends*. Norwood, N.J: Ablex Publishing Corporation.

Trudgill, P. (2000) *Sociolinguistics: An introduction to Language and Society 4th ed*. London: Penguin books.

Trudgill, P. (2002). *Sociolinguistic Variation and Change.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Tuki (1990) *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*.Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

UNESCO's Participation in the World Youth Festival, Barcelona 2004
Maria-Helena Mueller, UNESCO Bureau of Strategic Planning, Section for Youth

Wachiuri (2005) Language and Spread of HIV/AIDS. Tasnifu ya M.A: Kenyatta University.

Wambua, R. S (2009) Variation In Dialect Use Of And Attitudes Towards Taboo Words And Euphemisms In Kikamba. Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa, University of Nairobi.

Wamitila, K. (2003a) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

----------- (2003b) *Kichocheo cha Fasihi.* Nairobi: Focus Books.

Wanner, L and Bateman, J.A (1990) *A Collocational Based Approach to Salience-Sensitive Lexical Selection*. In Proceedings of the Fifth International Natural Language Generation Workshop, pages 31-38, Dawson, PA, 1990.459

Wardhaugh, R. (1986), *Introduction to Sociolinguistics,* (2nd ed.), Cambridge: Blackwell

Wardhaugh, R (2002) *An introduction to Sociolinguistics.* (4thEd) Oxford: Blackwell Publishers.

Yule, G (1996) *Pragmatics.*New York: Oxford University Press.

KIAMBATISHO A: HOJAJI

UTAFITI WA MAELEZO YA MIKAKATI YA MATUMIZI YA LUGHA KWA VIJANA.

SEHEMU A: MAELEZO KUHUSU MTAFITIWA

1. Jinsia: _____ 2. Umri: _____ 3: kidato________ shule_____________

4 Umilisi wa lugha (jaza kulingana na hali yako).

□ Msemaji wa lugha zipi ___________ _____________ ____________

SEHEMU B: MAELEZO YA MIKAKATI YA MATUMIZI YA LUGHA

Maadili katika jamii ni jambo moja linalostahiwa sana, kustahiwa ambako humpelekea mtu kutazamwa kwa njia tofauti. Mambo fulanifulani huenda yakatokea na kukupelekea kukabiliana nayo kwa njia yako mwenyewe. Kama mwanafunzi wa Kiswahili utakabiliana vipi na maswala haya. (ELEZEA KATIKA USEMI HALISI)

<u>Methali.</u>

1) Kwa maoni yako waweza kusema nini kuhusu methali hizi.

a) Kufa kwa mkundu mavi hutawanyika.

b) Kufa kwa mdomo mate hutawanyika.

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

a) Ukimwiga tembo kunya utapasuka msamba.

b) Ukimwiga tembo kunya utapasuka mkundu.

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

2) Uvutaji wa sigara umefanyika mahali ulipo, Utamwambia vipi mvutaji ikiwa

a) Ni baba mzazi_______________________________________

b) Mwalimu wako_______________________________________

c) Mwanafunzi mwenzako_________________________________

d) Mgeni wako_________________________________________

e) Mtu usiyemjua______________________________________

3) Hedhi imempata mwanamke / msichana na ambapo tokeo hilo umeliona wewe. Utamfahamishaje anayehusika ikiwa

a) Ni mama yako____________________

b) Wewe ni mvulana umemuona msichana wa darasa lako____________________

c) Wewe ni msichana umemuona msichana wa darasa lako ____________________

d) Ni mwanamke anayemzidi mama yako kwa umri____________________

4) Unataka kwenda haja utamwelezea vipi

a) Mzazi wako____________________

b) Mwalimu____________________

c) Rafiki yako____________________

d) Rafiki yako wa jinsia tofauti____________________

5) Una uhitaji wa fedha na ni lazima uzipate, utamwambiaje unayetaka akusaidie ikiwa ni

a) Mzazi wako____________________

b) Rafiki yako ____________________

c) Ni mtu usiyemjua____________________

6) Unamtamani msichana / mvulana fulani utaanzaje habari zako?

____________________

7) Umemtembelea mgonjwa wa ukimwi, utaelezea hali yake vipi ikiwa unazungumza na

a) Mtu wa familia yake____________________

b) Mwalimu wako____________________

c) Rafiki yako____________________

d) Mgonjwa mwingine wa ukimwi____________________

e) Mgonjwa huyo____________________

8) Rafiki yako amefanya urafiki wa kimapenzi na mvulana / msichana unayeijua mienendo yake mibaya. Habari hii utaielezea vipi ikiwa unayemweleza ni

a) Mzazi wake ____________________

b) Mwalimu________________________________________

c) Mvulana / msichana anayefanya urafiki huo ____________________

d) Rafiki zako wengine__________________________________

9) Mwalimu / mwanafunzi wa kiume / kike ameingia darasani zipu ya suruali / skati ikiwa haijafungwa utamwelezea vipi ikiwa ni

a) Mwalimu wa kike ____________________________________

b) Mwalimu wa kiume____________________________________

c) Msichana / mvulana ambaye ni rafiki yako______________________

10) Umezipata habari za kifo cha mtu unayemjua, utazisema vipi ikiwa unayezungumza naye ni

a) Mzazi wako________________________________________

b) Mwalimu wako______________________________________

c) Mmoja wa familia yake ________________________________

d) Rafiki yako________________________________________

11) Wizi wa vifaa vya wanafunzi darasani unafanyika na wewe unamjua anayefanya hivyo, utaisema vipi habari hii kwa

a) Wazazi wa mwizl_____________________________________

b) Mwalimu__________________________________________

c) Mwenye kufanya kitendo hicho____________________________

d) Rafiki ya yule unayemjua kama mwizi________________________

e) Wanafunzi wengine darasani_____________________________

12) Mwanafunzi amepatikana akifanya mapenzi darasani utawambia vipi

a) Wazazi wa wahusika wa kitendo hicho________________________

b) Mwalimu___________________________________________

c) Rafiki za wahusika wa kitendo hicho_________________________

e) Mchumba wa mhusika__________________________________

13) Umekifanya kitendo cha kuudhi kama vile kushuta / kujamba mbele ya watu

hawa, utamwambiaje kama ni

a) Mzazi wako____________________

b) Mwalimu ____________________

c) Rafiki yako____________________

d) Ndugu / dada yako____________________

e) Mtoto mdogo wa jirani yako____________________

14) Umepigiwa simu na mchumba wako wa siri mkiwa na wazazi wako. Je Utawambia vipi wakitaka kujua simu imetoka kwa nani?

____________________

15) Umemkuta mama / dada yako akiwa ameketi vibaya nje ya nyumba yenu, Utamwambia vipi ikiwa unajua kuwa atapakaa mahali hapo kwa muda mrefu? Ikiwa ni

a) Mama yako____________________

b) Dada yako____________________

16) Njia unayopitia ni nyembamba na unaharakisha kwenda mahali pa dharura, ghafla watu wawili wamesimama na kuanza kuongea bila kujali hali yako. Utawaambia nini ikiwa ni

a) Wazazi wako____________________

b) Walimu wako____________________

c) Marafiki zako____________________

e) Watu usiowajua____________________

17) Umemkuta mwanafunzi wa darasa lako akimnajisi mtoto wa umri mdogo, utaisemaje habari hii kwa

a) Mzazi wake mtoto____________________

b) Mzazi wa anayekitenda kitendo____________________

c) Ushahidi kwa polisi____________________

d) Wanafunzi darasani____________________

18) Umemkuta mtu akikunya shambani / au karibu na nyumba yenu, utamwambia vipi ikiwa ni

a) Mzazi wako________________________________________

b) Jirani yako________________________________________

c) Rafiki yako________________________________________

d) Mtoto wa jirani yako__________________________________

e) Mtu usiyemjua______________________________________

19) Umeumia sehemu zako za siri utatumia jina gani kuzitajia kwa watu hawa

a) Mzazi wako________________________________________

b) Mwalimu wako______________________________________

c) Daktari____________________________________________

d) Rafiki yako________________________________________

e) Mtoto wa jirani yako__________________________________

20) Umekasirishwa na mtu vibaya sana na tusi huenda limekutoka, tusi lipi huenda likakutoka ikiwa umeudhiwa na

a) Mzazi wako________________________________________

b) Mtu mzee usiyemjua___________________________________

c) Mwanafunzi mwenzako__________________________________

d) Mtoto mdogo wa jirani__________________________________

NAKUSHUKURU SANA KWA KUSHIRIKI KWAKO